Nipashe
Jumamosi Oktoba 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580059
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Tucta yabariki viongozi wake kusimamishwa siku 90 zaidi

UKURASA 3




UKURASA 13

# CJ awarushia kombora majaji na mahakimu

**ASEMA** baadhi wanaruhusu wenzi wao, marafiki kuvunja sheria, kujinufaisha...*Endelea ukurasa 2*





Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakipita jirani na shimo kubwa lililopo katikati ya barabara ya Mtaa wa Lindi, eneo la Mnazi Mmoja, jijini humo jana, ambalo ni hatari kwa waenda kwa miguu na vyombo vya moto. **PICHA: JOHN BADI**

## KESI ARDHI YASHINDWA KUAMULIWA MIAKA 55

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## Kortini kwa tuhuma kuiba tausi wa Ikulu

UKURASA 2

**MICHEZO** MSUVA AZIDI KUKIMBIZA WAKITINGA NUSU FAINALI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# China yaunga mkono kuondolewa vikwazo taifa la Zimbabwe

**Romana Mallya na Mary Georfey**

CHINA imeunga mkono Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) chini ya mwenyekiti wake Rais John Magufuli, kutaka Zimbabwe iondolewe vikwazo vya kiuchumi bila masharti.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema jana katika taarifa yake kuwa nchi hiyo inaunga mkono msimamo huo.

Akizungumza jana katika kongamano maalum lililokuwa likizungumzia vikwazo vya kiuchumi na hatua ya maendeleo ya Afrika kwa kuangalia uzoefu wa Zimbabwe, Balozi huyo alisema umefika wakati kwa nchi hiyo kuondolewa vikwazo hivyo.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wakati wa kufunga kongamano hilo lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema hatima ya Bara la Afrika imo mikononi mwa waafrika.

Akimwakilisha Rais Magufuli, Dk. Mpango alisema

INAENDELEA UK. 8



Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Phaustine Kasike (kushoto), akimvisha cheo cha Mkaguzi Msaidizi wa Magereza ambaye ni mmoja wa wahitimu wa Mafunzo ya Maofisa Wakaguzi Wasaidizi wa Magereza ambaye amefanya vizuri zaidi, wakati wa sherehe za kufunga mafunzo ya uongozi daraja la pili katika Jeshi la Magereza mkoani Morogoro jana. **PICHA: MAGEREZA**

# CJ awarushia kombora majaji, mahakimu

**Na Hellen Mwango**

JAJI Mkuu wa Tanzania. Profesa Ibrahim Juma, amewarushia kombora majaji na mahakimu kwamba wanaruhusu ndugu zao na wenzi wao kutumia nafasi zao kujinufaisha.

Sambamba na hilo, amewataka majaji na mahakimu kulegeza masharti ya dhamana kwa Watanzania kwa sababu ni haki yao ya msingi kupata dhamana ikiwamo kuwaamini kupitia vitambulisho vyao.

Prof. Juma alitoa kauli hiyo jana wakati wa kuwaapisha Naibu Wasajili wa Mahakama na kuwakabidhi vitendea kazi Mahakimu Wafawidhi wapya katika viunga vya Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam.

Alisema wako baadhi ya ndugu wa majaji au mahakimu ambao wanavunja sheria kwa kuchukua mali za watu wengine kwa kutumia vyeo vya watumishi hao wa mhimili wa dola.

"Waheshimiwa majaji na mahakimu, unaweza kukuta mke au mume wa jaji au hakimu anatumia nafasi ya mume au mke wake kuliko hakimu au jaji mwenyewe mpaka anaogopeka katika jamii. Wako wanaochukua mali za wengine na kuvunja sheria kwa makusudi kwa kutumia migongo ya wenza wao. Hii si sawa kabisa na tuiache," alisema.

"Mahakama inawatuma kwenda kufanya kazi ya umma na si kuwa mawakili wa familia au watoa msaada wa kisheria bali kutoa haki. Kwa kufanya hivyo ni kukiuka maadili ya mhimili huu," aliongeza.

Jaji Mkuu alisisitiza kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria, hivyo wasitumie nafasi walizo nazo kuzungumza na wakuu wa vituo vya polisi kwa ajili ya kuondoa mashtaka kwa ndugu zao na kwamba hiyo ni kinyume cha sheria.

Aidha, aliwataka mahakimu kutokubali kuahirisha mashauri kwa hoja nyepesi zinazotolewa na waendesha mashitaka kwamba upelelezi wa kesi unaendelea au haujakamilika.

Prof. Juma alisema ni lazima mahakimu watumie nafasi zao kuwabana waendesha mashtaka ili waseme ni upelelezi gani unaofanywa ambao haukamiliki kwa kuwa ndio chanzo cha kutomaliza mashauri kwa wakati.

Pia aliwataka waendesha mashtaka kutokubali kutishiwa

INAENDELEA UK. 8


## KUMBUKUMBU



215474102

**Wilneza Mathew Mrema Baba yetu mpendwa,** leo umefikisha miaka mitatu tangu mwenyezi Mungu alipotwaa roho yako nzuri na kukupa pumziko la milele; hakuna mtu ajuae ni kiasi gani tunaumia mioyoni mwetu; hakuna anayejua maumivu ambayo tumejeruhiwa tangu kutwaliwa kwako baba yetu mpenzi; maisha hayajawahi kuwa sawa miyoyoni mwetu kumbukumbu yako inatukumbusha mema yako mazuri kwetu, upendo wa agape na mengi uliotuachia baba; Hakuna siku mpendwa Baba ipitayo bila kufikiria juu yako. Unakumbukwa sana na mke wako mpenzi Eva, watoto wako Lucy, Goodie, Irene, Denis, Monica, Sia, David, Walter, wajukuu wako, Kaka na dada zako, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na uongozi na wafanyakazi wa Network Freight Forwarders Ltd.


# Kortini tuhuma kuiba tausi wa Ikulu

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kujihusisha na genge la uhalifu, kukutwa na nyara za serikali ikiwamo ndege watatu aina ya tausi wa Ikulu ya Tanzania na kutakatisha fedha.

Washtakiwa hao ni David Graha, Mohammed Hatibu na Mohammed Mahamoud wote wakazi wa jijini Dar es Salaam na walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, kati ya Juni Mosi, 2015 na Oktoba 14, mwaka huu, waliratibu mipango ya uhalifu kwa kujihusisha na biashara ya ndege hao wenye thamani ya Dola za Marekani 1,500 (sawa na Sh.3,444,150).

Nchimbi alidai shtaka la pili, washtakiwa walikutwa na ndege watatu aina ya tausi wenye thamani hiyo ya fedha.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu, Oktoba 14, mwaka huu eneo la Mikocheni mshtakiwa wa tatu, Mahamoud, alikutwa na tausi hao.

Ilidaiwa katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa kati ya Juni Mosi, 2015 na Oktoba 14, mwaka huu, sehemu tofauti jijini Dar es Salaam, mshtakiwa wa kwanza na wa pili, walijipatia Sh. 300,000 wakati wakijua ni zao la kutakatisha fedha.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa katika tarehe za tukio la nne, mshtakiwa wa tatu alijipatia Sh.300, 000 huku akijua ni zao la kosa la kutakatisha fedha.

Hakimu Mwaikambo Alisema washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Nchimbi alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

HABARI KITAIFA

# Vigogo Tucta 'kifungoni' siku 90

Na Mary Geofrey

MKUTANO Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), umebariki vigogo wake wawili kuendelea kusimamishwa kazi kwa siku 90 ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Waliosimamishwa kazi ni Katibu Mkuu wake, Dk. Yahya Msigwa na Naibu wake, Jones Majura ambao wanatuhumiwa kwa ubadhilifu wa fedha na matumizi mabaya ya madaraka ikiwamo kuuza nyumba.

Rais wa Tucta, Tumaini Nyamhokya, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, alisema mkutano mkuu huo uliomalizika jana, uliridhia kusimamishwa kazi kwa viongozi hao hadi kamati inayochunguza tuhuma hizo itakapokamilisha kazi yake.

"Tuhuma ndiyo zinashughulikiwa lakini kikao cha shirikisho kimeridhia kusimamishwa kazi kwa wenzetu wakati tuhuma zikiendelea kushughulikiwa," alisema Nyamhokya.

Aliongeza kuwa mkutano huo uliridhia tuhuma hizo zishughulikiwe ndani ya siku 90 kwa mujibu wa katiba ya shirikisho hilo.

"Kamati zimeundwa kwa kushirikiana na viongozi wa wafanyakazi na vikao vyenye uamuzi ndivyo vitatoa uamuzi kuwa kama wamethibitika na makosa au hawana makosa," alisema.

Alipoulizwa kamati hiyo inawahusisha viongozi gani, alisema ni masuala ya ndani ya shirikisho na hawezi kuitaja kwa sababu ni masuala yanayoshughulika na maisha ya watu.

Alisema walitoa siku 90 ili kutoa muda wa kujiandaa na mkutano wa kuwakutanisha kwa ajili ya kutoa maamuzi yatakayotolewa na kamati husika.

Oktoba 11, mwaka huu, viongozi hao walisimamishwa kazi kwa muda ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili ikiwamo kuuza nyumba ya Tucta iliyoko Mafinga mkoani Iringa bila uamuzi wa vikao halali na bila kufanya tathmini ya jengo lenyewe.

Baada ya kusimamishwa kwa viongozi hao walikuwa wakisubiri uamuzi wa Baraza Kuu la Uongozi na Mkutano Mkuu ambao ulifanyika kwa siku mbili jijini Dar es Salaam ambao ulibariki kuendelea kusimamishwa wakati wakisubiri hatima yao.

Mkutano huo mkuu ulitanguliwa na baraza kuu lililokutana Oktoba 21 na 22, mwaka huu.



Muuza maji akitembeza kwa kutumia mkokoteni unaokokotwa na Punda wakati akisaka wateja katika eneo la Vijibweni, Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. Dumu moja la lita 20 linauzwa kwa bei ya 500/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kesi yadumu miaka 55 bila hukumu

Na Happy severine, BARIADI

ASASI ya Legal Service Facility (LSF) inayotoa msaada wa kisheria (LSF) imeshangazwa kukutana na kesi za ardhi zilizochukua muda mrefu mahakamani katika Mkoa wa Simiyu, iliyodumu kwa miaka 55 na bado haijatolewa hukumu.

Mbali na kesi hiyo, asasi hiyo imeeleza kuwa imekutana na kesi nyingi ambazo zilianza muda mrefu huku walalamikaji wakiwa bado wadogo lakini mpaka sasa wamekuwa wazee na hazijatolewa uamuzi.

Mkurugenzi wa Miradi wa LSF, Scholastica Jullu, alisema hayo jana wakati wa kilele cha Wiki ya Msaada wa Kisheria Kitaifa iliyofanyika mjini hapa.

Alisema sababu kubwa ambayo wamegundua kwa kesi hizo kuchukua muda mrefu bila ya kutolewa hukumu ni walalamikaji kutokufuata utaratibu wa kufungua mashauri sehemu sahihi.

"Kuna kesi moja ina miaka 55 mahakamani. Ni kesi ya ardhi mpaka sasa haijafika mwisho lakini tumekutana na watu kesi yao ilianza toka wakiwa watoto lakini leo ni wazee bado haijamalizika," alisema Jullu.

Alisema walichogundua katika wiki hiyo, bado elimu ya kisheria inahitajika kwa kiwango kikubwa kwa wananchi na wasaidizi wa kisheria.

"Tumebaini kuwa wananchi wengi wamekuwa hawana uelewa wa sehemu ipi sahihi kesi zao za ardhi zinatakiwa kuanzia au ngazi gani waanzie ili kupata haki yao kwa wakati," alisema.

Jullu pia alisema wamekutana na kesi nyingi ambazo zimetolewa uamuzi lakini bado hukumu haijakazwa hali ambayo walalamikaji wanaendelea kulalamika.

Ofisa Programu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Grolia Baltazar, alisema kesi nyingi ambazo zinahusu migogoro ya ardhi zinatokea pale baba wa familia anapofariki dunia.

Alisema katika familia ambazo mama ametangulia mbele za haki, migogoro hiyo haijitokezi, hali ambayo alisema elimu ya kuandika wosia inahitajika zaidi kwa wananchi.

Naye Msajili wa Watoa Huduma wa Msaada wa Kisheria, Felister Mushi, kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, alisema kwa muda wa wiki moja wametoa huduma kwa zaidi ya watu 1,000.

" Kwa watu wote hao wengi walikuwa na kesi za ardhi, lakini nyingi ziko mahakamani. Tumegundua elimu ya kisheria inahitajika zaidi kwa wananchi," alisema Mushi.

Akifunga maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, alizitaka asasi za msaada wa kisheria kwenda zaidi kwa wananchi hasa maeneo ya vijijini kwa ajili ya kuwapatia elimu ya sheria mbalimbali.

# Polisi wazuia mkutano wa Msigwa

Na Enock Charles

JESHI la Polisi mkoani Iringa, limezuia mkutano wa Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, kwa madai ya kutokuwapo kwa askari wa kutosha wa kulinda mkutano huo.

Taarifa za kuzuiwa kwa mkutano huo zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii, ikionyesha barua ya zuio kutoka polisi. Mkutano huo ulikuwa ufanyike katika viwanja vya Mwembetogwa.

Kamanda wa Polisi Mkoani Iringa, Juma Bwire, alisema marufuku hiyo ilitokana na kutokuwapo kwa askari wa kutosha kwa kuwa wako kwenye usimamizi wa mitihani ya kidato cha nne, kidato cha pili na darasa la nne pamoja na kuwapo kwa taarifa za kiintelijensia juu ya kutokea vurugu na kusababisha uvunjifu wa amani.

Akizungumza na gazeti hili lililotaka kupata ufafanuzi zaidi, Kamanda Bwire alisema atalitolea ufafanuzi suala hilo baadaye lakini mpaka gazeti hili linakwenda mitamboni halikupata ufafanuzi huo.

"Ni kweli amezuiwa kufanya mikutano, ninaandaa taarifa nitajitolea ufafanuzi baadaie," alisema Kamanda Bwire.

Akizungumzia kuhusu kuzuiwa mikutano yake, Msigwa alisema hiyo ni kinyume cha sheria kwa kuwa Mbunge hutakiwa kutoa taarifa ili kuhakikisha usalama wa mikutano yake na si kuomba ruhusa kwa jeshi hilo.

"Mimi ni mbunge na ile ndiyo kazi yangu. Sasa kazi yao ni kulinda mikutano yangu ili pasitokee vurugu na si kuzuia. Hawa tatizo wanaogopa kwa sababu walishawadanganya wakubwa wao kuwa Chadema Iringa haipo sasa wanaogopa nyomi ya watu watakaokuja kwenye mkutano wangu," alisema Msigwa.

Barua hiyo ya Jeshi la Polisi Iringa iliyosambaa katika mitandao ya kijamii ilieleza sababu ni uchaguzi wa serikali za mitaa na iwapo mkutano huo utafanyika, itakuwa sawa na kufanya kampeni.

"Kuna tarifa za kiintelejensia kuwa kuna makundi ya watu wanajiandaa kutumia fursa ya mkutano kufanya vurugu, hii itasababisha uvunjifu mkubwa wa amani," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Barua hiyo ni ya Octoba 24, mwaka huu, ikijibu barua ya Msigwa ya Octoba 22, mwaka huu, aliyeomba kufanya mkutano leo.

# Mjane aamuriwa apelekwe mahabusu

**Na Hellen Mwango**

HAKIMU Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Kevini Mhina, jana alisisitizia upande wa Jamhuri katika kesi inayomkabili mshtakiwa Elizabeth Balali (54) kuhakikisha anapelekwa gerezani na si vinginevyo mpaka Novemba 7, mwaka huu, kesi yake itakapotajwa.

Amri hiyo aliitoa jana baada ya Wakuu wa Kituo cha Polisi Oysterbay, Mrakibu Msaidizi (ASP) Kazwenge na wa Kijitonyama, ASP Rajuwo, kufika na kuzungumza naye ofisini kwake mapema jana.

Hata hivyo, vigogo hao wa Polisi haikufahamika wamezungumza nini.

Elizabeth ambaye ni msimamizi wa mirathi wa mke wa marehemu Daudi Ballali, alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza akikabiliwa na kesi ya ujumumu uchumi ikiwamo ulaghai, kujipatia Sh. milioni 25 na kutakatisha fedha.

Jana Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika.

"Mshtakiwa apelekwe mahabusu. Nasisitiza tena mshtakiwa apelekwe mahabusu mpaka Novemba 7 kesi yake itakapokuja kutajwa tena,"alisema Hakimu Mhina.

Mapema juzi, mahakama hiyo iliamuru wakuu wa vituo hivyo kwenda kuieleza mahakama sababu gani mtuhumiwa huyo alipelekwa na kuwekwa kituo cha polisi Oysterbay na Kijitonyama, badala ya gereza la Segerea.

Katika kesi ya msingi, Simon alimsomea mshtakiwa huyo mashtaka yake kwamba kati ya Oktoba 19 na Desemba 21, 2017 jijini Dar es Salaam alijipatia Sh. milioni 25 kutoka kwa Dk. Roderick Kisenge kwa ulaghai.

Mshtakiwa anadaiwa kujifanya anamuuzia Dk.Kisenge eneo la mita za mraba 900 ambalo halijapimwa lililopo eneo la Boko Dovya, Kinondoni wakati akijua eneo hilo si lake.

Wankyo alidai katika kipindi hicho mshtakiwa huyo alipokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Dk. Kisenge kupitia akaunti yake iliyoko katika Benki ya CRDB wakati akijua fedha hizo ni zao la kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Baada ya kusomewa mashtaka, Elizabeth hakuruhusiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza makosa ya uhujumu uchumi.

Hakimu Mhina alimfahamisha mshtakiwa huyo kuwa licha mahakama kutokuwa na uwezo wa kuisikiliza kesi hiyo, pia shtaka la utakatishaji wa fedha halina dhamana.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika.

Hakimu alisema Kesi imeahirishwa hadi Oktoba 24, mwaka huu (jana) kwa ajili ya kutajwa na mshtakiwa alipelekwa rumande kituo cha polisi badala ya Segerea.

# Waziri aagiza viongozi ushirika kukamatwa

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, ameliagiza Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara kuwakamata viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika (Amcos) wanaotuhumiwa kukimbia na Sh. bilioni 1.2 za wakulima ambazo ni madeni ya korosho.

Masauni alitoa amri hiyo jana mkoani humo, wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Newala katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Stendi Kuu.

Alitoa amri hiyo baada ya kupokea ripoti ya jumla ya madeni wanayodai wakulima katika wilaya za Mtwara, Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba.

"Nilipofika hapa Mtwara jambo la kwanza nilimwuliza Kamanda wa Polisi wa hapa kuhusu utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa siku za hivi karibuni alipokuwa ziarani na kuagiza kukamatwa viongozi wawili wanaodaiwa fedha za korosho na wakulima," alisema.

Masauni alisema Kamanda amemwambia kuwa walitekeleza agizo hilo na viongozi hao wameanza kulipa fedha hizo.

"Rais kwenye ziara yake aliishia Wilaya ya Masasi lakini katika ripoti hapa inaonyesha katika wilaya zingine wakulima pia wanadai fedha nyingi. Nakuagiza Kamanda wa Polisi uwakamate viongozi wengine katika wilaya zilizobakia na hakikisha kiasi hicho cha fedha za wakulima hao kinalipwa," alisema Masauni.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Blasius Chatanda, inaonyesha vyama 61 vya ushirika bado vinadaiwa na wakulima katika wilaya za Mtwara, Masasi, Tandahimba na Newala kuanzia msimu wa korosho wa mwaka 2015/16 hadi 2017/18.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mkutano huo, baadhi ya wakulima wanaodai fedha zao waliiomba serikali kuhakikisha wanalipwa haki yao kwani madeni hayo yamechukua muda mrefu na kusababisha kuzorotesha shughuli zao za kuchumi na familia zikipata tabu.



Wanafunzi wakivuka barabara kwa tahadhari katika eneo la Tandale Muhalitan, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOHN BADI**

# Hukumu Malinzi, wenzake Nov. 17

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka (TFF), Jamal Malinzi na wenzake watatu kurudi uraiani au la itajulikana Novemba 7,mwaka huu watakaposomewa hukumu.

Malinzi na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa USD 173,335.

Uamuzi huo ulisomwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde aliyesikiliza kesi hiyo kuwa na udhuru.

Hakimu alisema baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi wa pande zote mbili, mahakama yake itatoa hukumu mwezi ujao.

Wakili wa Serikali Ester Martin alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kupanga tarehe ya hukumu na kwamba upande wa Jamhuri uko tayari.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itasomwa hukumu tarehe iliyopangwa na kuamuru washtakiwa warudishwe mahabusu.

Mapema mahakamani hapo, upande wa Jamhuri uliita mashahidi 15 na vielelezo tisa kuthibitisha kesi hiyo na utetezi walileta mashahidi wanne kupangua tuhuma hizo.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya

Katika kesi hiyo mashahidi 15 wa upande wa Mashtaka walitoa ushahidi na tayari aliyekuwa Rais wa TFF Jamal Malinzi ameanza kujitetea mahakamani hapo.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wako rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha kuwa miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku Frola akiwa nje kwa dhamana.

## HABARI KITAIFA




Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi, akizugumza wakati wa hafla ya kupokea msaada wa mifuko 600 ya saruji kutoka Benki ya NBC kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu jijini humo jana. Katikati ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa na (kulia) ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Kusini, Salema Kileo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka yakiri bodaboda pasua kichwa

**Na Anthony Gervas**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra), imekiri kuwa udhibiti wa usafiri wa pikipiki maarufu bodaboda, bado ni changamoto na pasua kichwa.

Kwa mujibu wa Latra, changamoto hiyo inatokana na ongezeko la bodaboda mpya kila siku, hivyo hata utoaji wa elimu ya udhibiti wa matumizi ya barabara, sheria na kanuni kuwa ngumu zaidi.

Akizungumza juzi na Nipashe jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri Ardhini wa Latra, Johansen Kahatano, alisema mamlaka hiyo bado inakabiliwa na changamoto hiyo kwa upande wa huduma za bodaboda.

Kwa mujibu wa Kahatano, changamoto hiyo inatokana na madereva wengi kutojua sheria na kanuni za usalama barabarani.

"Udhibiti wa huduma za usafiri wa bodaboda barabarani bado ni mgumu kutokana na tabia za madereva, uelewa wao, elimu, utumiaji wa vyombo hivyo na utambuzi wao.

Hii kwa kiasi kikubwa inatokana na kila siku kuongezeka kwa bodaboda mpya barabarani," alisema Kahatano.

Alisema waendesha bodaboda walio wengi hawazingatii sheria na kanuni za usalama barabarani, hivyo kusababisha kuwapo changamoto nyingi zinazosababisha ajali barabarani na madhara kwa abiria yasiyokuwa ya lazima.

Kutokana na hali hivyo, madereva wengi wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kutozwa faini na wengine kuwafikisha mahakamani.

Alisema ili kupambana na changamoto hiyo, Latra imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuwatambua bodaboda kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kutoa elimu kwa madereva na wadau wengine ambao ni watumiaji wa barabara.

Ili kupunguza changamoto hizo, Kahatano alisema Latra imekusudia kuweka mikakati kabambe ya kuhakikisha wamiliki wa bodaboda wanatambuliwa na vyombo vyao kusajiliwa kwa kutumia mfumo wa kisasa zaidi ili wanapotenda kosa madereva wao iwe rahisi kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani.

# Majaliwa atoa neno wawekezaji Russia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameutaka ubalozi wa Tanzania nchini Russia kuratibu mipango ya wafanyabiashara wa nchi hiyo wanaokusudia kuwekeza nchini kwa kuwaunganisha na taasisi na wizara husika ili wawekeze kwa kuzingatia maslahi ya taifa.

Majaliwa alitoa agizo hilo juzi baada ya kugundua kuwapo wafanyabiashara wengi wa Russia wanaokusudia kuja Tanzania kwa ajili ya kuangalia maeneo ya uwekezaji pamoja na kutafuta wafanyabiashara wa Kitanzania watakaoungana nao katika uwekezaji.

"Tayari miadi imekwishawekwa ya kuwakaribiasha wawekezaji wa Russia kuja Tanzania kwa ushawishi wangu mwenyewe pamoja na ushawishi wa wafanyabiashara wa Tanzania, hivyo nisingependa wafanyabiashara hao wasumbuliwe au kukatishwa tamaa katika kutimiza nia yao hiyo," alisema majaliwa.

Alisema mkutano baina ya wakuu wa nchi na serikali kutoka mataifa ya Afrika na Russia uliomalizika juzi, ulilenga kujenga uhusiano mzuri katika nyanja mbalimbali hususan za kiuchumi.

Akizungumza baada kumalizika mkutano huo kwenye ukumbi wa Olympic Park wa Sochi nchini Russia, Waziri Mkuu alisema Russia imeutumia mkutano huo kueleza bayana maeneo ambayo iko tayari kushirikiana na Afrika katika kuwekeza kwa faida ya pande zote mbili.

Waziri Mkuu aliyataja maeneo hayo kuwa ni uuzaji wa zana za kilimo kama vile matrekta, mafuta, gesi na madini, ujenzi wa miundombinu hasa reli, masuala ya elimu hasa utoaji wa nafasi za mafunzo nchini humo.

Alisema kwa upande wake, Tanzania imejinadi vizuri ikiongozwa na yeye mwenyewe kwa kuwa alifanya mazungumzo na viongozi wa kampuni nane za Russia na kuzishawishi kuwekeza nchini na zote zilikubali kufika Tanzania mapema iwezekanavyo.

"Viongozi wa kampuni zote nilizopata nafasi ya kuzungumza nao wamesema wako tayari kuja nchini ili kufanya mazungumzo na serikali pamoja na wafanyabiashara wazalendo ambao wako tayari kuungana na wafanyabiashara hao katika kuwekeza nchini Tanzania," alisema.

Waziri Mkuu alisema viongozi hao walimweleza maeneo ambayo wanaamini kuwa wanafanya vizuri na wangependa kupata kibali cha kuwekeza Tanzania baada ya mazungumzo yao na serikali. Pia walieleza ni kwa namna gani taifa litanufaika na uwekezaji wao.

Alisema tayari wafanyabiashara binafsi 18 wa Tanzania walijitokeza kushiriki katika mkutano huo na walifanya kazi kubwa na nzuri ya kuwahabarisha wenzao wa Russia kuhusu mazingira mazuri ya kuwekeza hasa baada ya serikali kuondoa kero, kanuni na taratibu ziliokuwa zikiyafanya mazingira ya uwekezaji kuwa magumu.

Jana, Majaliwa aliondoka Russia kwenda Azerbaijan ambako pia atamwakilisha Rais John Magufuli katika mkutano wa siku mbili wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote.



# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Yanga ikitekeleza haya Pyramids itafia Kirumba

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga watashuka dimbani kesho kwenye mechi ya kwanza ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Yanga imeangukia Kombe la Shirikisho baada ya kutolewa na Zesco ya Zambia kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo kesho itaikaribisha Pyramids ya Misri katika Uwanja wa CCM Kirumba kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya Kombe hilo la Shirikisho.

Na ili Yanga iweze kufuzu hatua hiyo, itahitaji kupata matokeo ya jumla katika mechi mbili, ya kesho na zitakaporudiana wiki mbili zijazo nchini Misri. Tayari Pyramids wamewasili nchini kwa ajili mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa ngumu kwa timu zote, lakini Yanga ikitarajiwa kutumia vema uwanja wake wa nyumbani kabla ya kuwafuata Wamisri hao kwao.

Tunatambua Pyramids ambayo kwa sasa inaongoza msimamo wa Ligi Kuu Misri ikiwa na alama 11 baada ya kushuka dimbani mara tano mechi moja mbele dhidi ya Zamalek yenye pointi 10 katika nafasi ya pili, si timu ya kubeza hata kidogo na inaundwa na nyota wengi kutoka Amerika Kusini.

Miongoni mwa wachezaji nyota wanaounda kikosi cha Pyramids ni pamoja na nyota kutoka Brazil na Colombia ambao gharama ya kuwanunua inaelezwa kuwa zaidi ya Sh. bilioni 70 za Tanzania, jambo linaloashirikia ni wa daraja la juu.

Hata hivyo, Nipashe tunaamini gharama ya mchezaji haiwezi kuwa sababu kwa Yanga kuihofia Pyramids katika mechi hiyo ya kesho itakayoamua hatima yao kwenye michuano ya kimataifa baada ya wawakilishi wengine wa Tanzania, Simba, Azam, KMC, KMKM na Malindi kutolewa katika kinyang'anyiro hicho.

Ni kweli tunakubaliana na gharama ya mchezaji mara nyingi inatokana na ubora wake, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kujiaminisha kuwa inaweza kuibeba Pyramids mbele ya Yanga ambayo itakuwa katika uwanja wake wa nyumbani ikiungwa mkono na mashabiki wake. Tulishuhudia msimu uliopita kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika Simba ikiwazima ndugu wa Pyramids, Al Ahly ya Misri katika Uwanja wa Taifa kwa bao 1-0, wakati wengi wakiamini wawakilishi hao wa Tanzania wangeangukia tena pua baada kuchezea kichapo cha mabao 5-0 ugenini.


Wengi walijiamisha kuwa Simba ingechezea tena kichapo nyumbani na imani hiyo ikiongezeka kutokana na Al Ahly kuundwa na wachezaji bora na ghali ambao mmoja tu gharama yake ilikuwa ni mara tano zaidi ya bajeti ya kikosi kizima cha Wekundu wa Msimbazi hao.

Hivyo kwa maandalizi ambayo Yanga imefanya ikiwa ni pamoja na kuwavuruga wapinzani wao kisaikolojia kwa kuwapeleka Uwanja wa CCM Kirumba hatua iliyozua hofu kwao kuwa wanapelekwa 'machinjoni' kunaweza kuwapa wawakilishi wetu hao matokeo mazuri. Kinachotakiwa kwa Yanga si tu kupata matokeo bali pia kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo huku ikiepuka kutoruhusu bao la ugenini kwa wapinzani wao ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele watakaporudiana wiki mbili zijazo nchini Misri. Nipashe tunaikumbusha Yanga kuwa makini na mashambulizi ya kushtukiza na kucheza mchezo wa kasi mwanzo mwisho kwani falsafa za timu za Kiarabu mara nyingi ni kucheza taratibu na kushambulia kwa kushtukiza huku wakipoteza muda mwingi wakiwa ugenini.

Lakini pia mashabiki wa Yanga na Watazania kwa ujumla, hawana budi kuitumia vema nafasi yao ya kuwa mchezaji wa 12 timu inapocheza nyumbani kwa kuishangilia mwanzo mwisho huko wakiwaozomea wachezaji wa Pyramids kila wanapogusa mpira.

Tunataka kuona Yanga ikisonga mbele ili kutetea nafasi ya Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao, hivyo hili si jukumu la wawakilishi hao tu, bali Watanzania wote hawana budi kuungana katika kuhakikisha Yanga inasonga mbele katika michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Barnabas Maro

## Sihadaike na rangi...

**"SIHADAIKE** na rangi tamu ya chai ni sukari." Maana yake usidanganyike na rangi ya chai, kwani utamu wake hutokana na sukari.

Hii ni methali ya kutumiwa kumkanya mtu asipumbazike au asivutwe na sifa za nje za kitu ila akichunguze kitu hicho kwa undani, kwa lengo la kupata na kujua uhakika wake ili kujiridhisha.

Kadhalika, maana ya "Feli mbaya" ni kisirani au mkosi. Mfano, timu zetu za kandanda zimekuwa na feli mbaya katika michezo yao, ndani na nje ya nchi. Hapana shaka hali hii yasababishwa na kuwategemea sana wachezaji wa kigeni na kuwadharau wa kwetu.

Baadhi ya wachezaji wa kigeni waliosajiliwa na klabu zetu hawamo katika timu za mataifa yao. Hata baadhi ya wachezaji wetu wana uwezo zaidi yao, lakini hawathaminiwi!

Kadhia hii yatokana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutokuwa na utaratibu wa kuwaandaa vijana watakaokuwa wachezaji wa taifa miaka ijayo. Laiti kungekuwa na utaratibu wa kuwatafuta wachezaji vijana nchini, hapana shaka Tanzania ingekuwa moja ya nchi zilizoendelea kwa kandanda Afrika.

Nashauri timu za taifa zijitoe kwenye michezo ya kimataifa kwa muda wakati juhudi za kupata vijana stahiki zikifanywa nchi nzima.

Watakaokwenda mikoani kutafuta vijana wenye vipaji, wasiwe Watanzania bali wawe wataalamu kutoka nje ya nchi waliobobea katika kandanda. Nashauri hivyo ili kuondoa U-simba na U-yanga walionao viongozi wetu wakiwamo waamuzi kuanzia wilaya, mikoa mpaka TFF!

Wakati hilo likiendelea, TFF iwe mbioni kuandaa eneo maalumu la kuwapa mafunzo vijana watakaochaguliwa na isiwe Dar es Salaam.

Aidha, asiruhusiwe mtu yeyote kuingia eneo litakalotumiwa kuwafunza vijana hao ili kuepuka ghiliba (udanganyifu wenye nia ya kujinufaisha) Simba na Yanga kwa lengo la kuwasajili.

Eneo hilo liwe na madarasa yatakayotumiwa kuwapa vijana hao elimudunia ili watakapokamilisha mafunzo yao ya kandanda, pia wawe wameelimika. Hii itawasaidia kujua lugha ngeni, hasa Kiingereza ambacho chazungumzwa duniani kote. Itawasaidia wanapotakiwa na timu za ughaibuni.

Kwa njia hii twaweza kupata vijana wazuri watakaounda timu zetu za taifa kwani kutokana na umahiri wao watataua ndege wawili kwa mpigo. Kucheza kwenye timu zetu za taifa na uwezekano mkubwa wa kusajiliwa na timu za nje. Hii itakuwa faida kubwa kwao na nchi pia.

Wakati hayo yakiendelea, klabu zilazimishwe kuwa na viwanja vyao vya mazoezi na mechi kama ilivyo kwa wenzetu. Viwanja hivyo viwe na mambo muhimu kama mabwawa ya kuogelea, vyumba vya mazoezi ya viungo, zahanati, kantini, vyumba vya wachezaji n.k.

Utaratibu huo utaokoa fedha za klabu zinazotumika kukodi viwanja vya mazoezi na hata mechi za ligi na za kimataifa. Ndivyo zilivyo timu za wenzetu.

Kuendelea kutegemea wafadhili kumepitwa na wakati. Tangu Yanga na Simba zianzishwe miaka ya 1935 na 1936, zimekuwa zikiwategemea wafadhili waliokuwa na malengo maalumu, ama kukuza biashara zao au kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa nchini.

Hata hivyo, waliokuwa viongozi wa klabu hizo nao walitumia nafasi hiyo kujinufaisha kwa kile walichosema 'kupiga hela!' Matokeo yake wafadhili walishtuka na kujiondoa taratibu huku klabu zikiendelea kudorora bila maendeleo yoyote!

Kama Yanga na Simba zingekuwa na mipango madhubuti ya kuimarisha klabu zao, leo Tanzania ingekuwa mfano wa kuigwa Afrika Mashariki. Badala yake, Azam iliyoanzishwa na mtu aitwaye S.S. Bakhresa ndiyo inayokuwa mfano kwa Yanga na Simba zilizoanzishwa miaka 85 iliyopita!

Ni vema kukumbusha kuwa Bakhresa alikuwa mfadhili wa Simba wakati ule akifanya biashara ya nyama na hoteli. Alipoona mambo hayaendi alivyotaka, akaamua kujitoa na kujiandaa kuunda timu yake.

Sasa Azam FC ndio mwalimu wa wakongwe, Yanga SC na Simba SC. Wakati timu hizi zikishituka na kuanza taratibu za kuwa na viwanja vyao, Azam FC inatafuta njia zingine za kujiendeleza zaidi.

Haitashangaza kama atakuwa na mpango wa kununua ndege ya kuwasafirisha wachezaji wake kwenye michezo ya Ligi Kuu humu nchini na ya kimataifa. Penye nia pana njia.

Nampa kongole Bakhresa kwa methali hii: "Atanguliaye kufika huchagua pa kukaa." Maana yake anayefika mahali fulani mapema huweza kuchagua mahali pa kukaa kabla ya wengine hawajafika.

Methali hii hutumiwa kutuhimiza tuwe na tabia ya kuwahi vitu mapema. S.S. Bakhresa aliwahi kufika; na waliomtangulia (Yanga na Simba) sasa wanamwangalia kwa macho ya huruma yenye tafsiri ya "laiti tungejua ...!"

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Jangili amfyeka mkono askari wanyamapori

**Na Mwandishi Wetu**

ASKARI wanyamapori Deus Mwakajegere (35), amedaiwa kukatwa mkono na jangili aliyemkamata akichunga ng'ombe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Jangili huyo anadaiwa alikamatwa ndani ya hifadhi hiyo akichunga ng'ombe akitokea kijiji cha Bisarara. Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana jana na kuthibitishwa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi-Mawasiliano, Pascal Shelutete, askari huyo alijeruhiwa akiwa katika doria.

Shelutete alisema tukio hilo lilitokea Octoba 23, mwaka huu na kwamba amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando kwa matibabu zaidi.

"Jangili aliyehusika na tukio hilo tunaendelea kumtafuta ili afikishwe mbele ya sheria, alisema.

Vitendo vya ujangili katika hifadhi za taifa nchini vilikithiri kati ya mwaka 2013 na 2016 lakini vilipungua baada ya serikali kuanzisha jeshi usu ndani ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Katika kipindi hicho, watu 5,752 walikamatwa wakijihusisha na vitendo vya ujangili huku kesi 2, 338 zikifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini.

Sambamba na hilo, bunduki 399 na risasi 382 zilikamatwa katika hifadhi zikiwa zinatumika kwa matukio hayo. Pia silaha 67 za jadi zilikamatwa.



Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa kampuni ya Selecom, Baguma Ambari (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu jinsi ya kulipia mafuta kwa kutumia Mastercard, kwa wamiliki magari wanaotumia vituo vya mafuta ya Puma Tanzania, ambapo mteja atarudishiwa asilimia 5 ya fedha kwa kutumia kadi hiyo. Kutoka (kulia) ni mfanyakazi wa Puma, Khamis Ali, Mkurugenzi Mtendaji wa Puma, Dominic Dhanah na Mkurugenzi Mtendaji wa Selcom, Sameer Hirji. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sababu viziwi kushindwa kufaulu zatajwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWALIMU mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija, manispaa ya Shinyanga, Selemani Kipanya, amataja sababu ya wanafunzi wasiosikia (Viziwi) kushindwa kufanya vizuri kwenye matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka huu.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, wanafunzi hao hawakufanya vizuri kutokana na shule kukabiliwa na upungufu wa walimu wenye taaluma hiyo.

Kipanya alibainisha hayo juzi kwenye hafla fupi iliyoandaliwa na Ofisa Elimu Kata ya Ibinzamata, Mackline Shija, kwa ajili ya kuzipongeza shule zake mbili ambazo anasimamia kitaaluma kutokana na kufanya vizuri. Shule hizo ni Buhangija na Ibinzamata.

Shule ya Buhangija inafundisha wanafunzi wa kawaida na wenye ulemavu mbalimbali, wakiwamo wenye ualbino, wasioona na viziwi na katika matokeo ya darasa la saba, wanafunzi wenye ualbino na wasioona, wote wamefaulu kwenda kidato cha kwanza.

Alisema wanafunzi wenye ulemavu waliofanya mtihani wa darasa la saba walikuwa 18, wakiwamo wenye ualbino sita ambapo walifaulu wote, wasioona wanne nao wamefaulu wote na wasiosikia wanane ambao watano kati yao wamefaulu. "Shule yetu hii inafundisha wanafunzi wa kawaida pamoja na wenye ulemavu mbalimbali na tunakabiliwa na upungufu wa walimu wenye taaluma ya kufundisha hawa walemavu hasa wasiosikia (niziwi). Hiyo ndiyo sababu ya kufanya vibaya mitihani yao ya darasa la saba na kushindwa kufaulu wote,"alisema Kipanya.

"Wanafunzi hawa wasiosikia shuleni hapa wako 74 kwa sasa lakini tuna walimu watatu tu wenye taaluma hiyo, hivyo naiomba serikali ituletee walimu wa kutosha ili tuondokane na changamoto hii ya wanafunzi viziwi kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani hayo ya kuhitimu elimu ya msingi," aliongeza. Naye Ofisa Elimu wa Shule Maalumu za Msingi katika Manispaa ya Shinyanga, Edward Mdagata, alikiri kuwapo kwa tatizo la walimu wenye uwezo wa kufundisha wanafunzi hao wenye ulemavu mbalimbali hasa viziwi.

Kutokana na changamoto hiyo, alibainisha kuwa tayari wameshatuma maombi ya walimu hao na wanasubiri majibu.

# Kiwanda chaomba suluhu mgogoro wa ardhi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

KIWANDA cha kusindika nyama cha Happy Sausage cha jijini Arusha, kimeiomba serikali kuingilia kati mgogoro wao na Halmashauri ya Jiji la Arusha unaokwamisha kukua kwa uzalishaji, hivyo kushindwa kufikia soko la kimataifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda hicho, Andrew George, alisema jana kiwandani hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuelezea shughuli zinazofanywa na kiwanda na changamoto zao.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Arusha imeendelea kukwamisha juhudi za ukarabati wa kiwanda hicho kwa kukataa kutoa kibali cha ukarabati wakati serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja Bodi ya Nyama wameshatoa maelekezo ya kufanyika kwa ukarabati.

Mwenyekiti huyo alisema hatua hiyo imetokana na mgogoro wa muda mrefu unaofikia miaka minane kati ya pande hizo kuhusiana na umiliki wa ardhi wa eneo ambalo hadi sasa kila upande unavutia kwake.

"Kiwanda kimeshindwa kufikia malengo ya uzalishaji kwa kukwamishwa kufanya ukarabati hali hiyo ambayo serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikikitaka kiwanda kufanya ukarabati,' alisema.

Alisema kuwa kiwanda hicho licha ya misukosuko hiyo, kimewalipa wafugaji wanaouza mazao ya mifugo zaidi ya Sh. Bilioni tisa na kulipa kodi ya serikali, leseni, tozo na vibali mbalimbali kwa jumla ya Sh. bilion 2.2 ndani ya miaka sita.

George alisema masoko yao makubwa ya kuuza bidhaa wanazozalisha ni ya ndani ya nchi katika mikoa yote nchini kupitia hoteli mbalimbali za kitalii na maduka ya rejareja ya nyama. Aliongeza kuwa mpango wao kwa sasa ni kuelekea kwenye masoko ya nje ya nchi yakiwamo ya Afrika ya Mashariki pamoja na Jumuia ya maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

# CJ awarushia kombora majaji, mahakimu

INATOKA UK. 2

chochote na kwamba ikitokea hakimu akifanya hivyo, mara moja wampeleke kwa mtendaji mkuu kwa sababu kitendo hicho ni kukiuka maadili.

Ili kufanya kazi zao kwa weledi na umahiri, aliwataka wapitie mabadiliko mbalimbali ya sheria na kwamba kwa kufanya hivyo kutawasaidia kumaliza kesi kwa wakati ili kuimarisha utoaji haki.

Kuhusu dhamana, Prof. Juma alisema mahakimu wasiwe wagumu kutoa dhamana kwa Watanzania kwa sababu ni haki zao na wasizuie kwa matakwa yao binafsi.

Alisema mshtakiwa atakuwa na wadhamini wenye vitambulisho vya uraia, hivyo wapewe dhamana na endapo atakimbia maana yake atajihukumu kwa kukimbia uraia wake. Akizungumzia sheria ya makubaliano, Jaji Mkuu alisema sheria hiyo imekataza makosa machache na kwamba haitumiki kwa mashtaka ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi pekee.

Alifafanua kuwa sheria hiyo ambayo mshtakiwa anaingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), inapaswa kutumika kwa makosa mengi zaidi kwa kuwa anaamini itasaidia kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani.

Manaibu Wasajili walioapishwa ni Happiness Ndesamburo, Warsha Ng'humbu, Elizabeth Nyembele, Niku Mwakatobe, Arnold Kirekiano, David Ngunyale, Flora Mtarania, James Kareyamaha, Magdalena Ntandu, Chiganga Tengwa na Godfrey Isaya.

Mahakimu Wafawidhi waliokabidhiwa vitendea kazi ni Hassan Makube, Gadiel Mariki, Ebiseeza Kalegeya, Maira Kasonde, Martha Mahumbuga, Elimo Massawe, Silvia Lushashi, Monica Ndyekobora, Gabriel Ngaeje na Venance Mlingi.



Aliyekuwa rais wa TFF, Jamali Malinzi, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayomkabili na wenzake watatu ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa USD 173,335 kuahirishwa hadi Novemba 7, mwaka huu watakaposomewa hukumu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# China yaunga mkono kuondolewa vikwazo taifa la Zimbabwe

INATOKA UK. 2

ni lazima nchi za Afrika zijielekeze kupanua wigo wa kiuchumi hasa katika uzalishaji na masoko.

"Zamani tulikuwa tunajua uchumi ni Marekani na Ulaya lakini siku hizi uchumi mkubwa uko mashariki.

Zipo China ambao wanatuunga mkono, Urusi (Russia), Brazil kwa hiyo tukitambua hili na kwamba kuna ushindani mkubwa katika kulinda maslahi ya kila taifa, vikwazo vinabadilika kadri muda unavyopita," alisema.

Alisema ni muhimu Afrika ichukue fursa hiyo ya kuhama kwa nguvu za kiuchumi duniani, kujihami dhidi ya madhara ya vikwazo ambavyo vinawekewa nchi kama Zimbabwe.

Dk. Mpango alisema shida iliyopo sasa ni uhuru wa kiuchumi, fikra za utegemezi na uhisani bado zinaelemea Afrika na kutaka zipigwe vita.

Alisema Afrika lazima izingatie utawala wa sheria na misingi thabiti ya menejimenti ya uchumi bila kusahau uhalisia katika nchi.

"Kamwe tusisalimu amri kwa wale wanaojaribu kupinda mikono yetu na kuhatarisha uhuru wetu wa kujitawala. Lazima tuwe mfano wa kuwekeza mitaji na ujuzi katika nchi zetu badala ya kuikimbizia nje ya nchi. Afrika hatuna budi kushikamana," alisisitiza.

Dk. Mpango alisema mshikamano wa kweli bado ni dhaifu wakati mataifa makubwa yanapojitetea kwa hoja, waafrika hawajibu mapigo. Alitaka vikwazo vya kiuchumi vigeuzwe kuwa fursa ya kukuza biashara na uwekezaji miongoni mwa nchi ndani ya bara hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema msimamo wa SADC ni Zimbabwe iondolewe vikwazo bila masharti.

"Rais wa Zimbabwe amesema yupo tayari kuanza kuwafidia kuwarudishia fedha baadhi ya walowezi wa mashamba, huu si uamuzi wa kawaida," alisema.

Waziri Mkuu Mstaafu, Joseph Warioba, akichangia mada zilizotolewa kwenye kongamano hilo ikiwa ni pamoja na msimamo wa SADC alisema: "Nadhani kwa tamko hilo wanawasha moto upya."

"Msimamo wa SADC usiishie SADC uenezwe kwa sababu kuna ukoloni mamboleo. Zimbabwe mkiondoa vikwazo peke yake haitoshi lazima muwasaidie wapate jawabu la suala la ardhi na mtalipata pia Afrika Kusini," alisema.

Warioba alisema lazima waangalie kwa nini sasa hivi imekuwa mtindo wa nchi zilizoendelea kuweka vikwazo kisha kutaka waingie kwenye majadiliano.

"Imekuwa ni mbinu ya kulazimisha nchi kukubali matakwa ya nchi kubwa. Unatoa vikwanzo kisha unasema tuzungumze, nchi za dunia ya tatu zimekaa kimya hazisemi chochote. Marekani anatoa vikwazo kwa Korea Kaskazini, kwa Iran kisha anasema wazungumze na sisi tumekaa kimya.

"Nadhani imefika wakati tuwe na msimamo. Kama tulivyopigania uhuru, tuwe na msimamo huu, utaratibu mpya wa ukoloni mamboleo," alisema.

Alisema kwa utaratibu huo wa nchi zilizoendelea, nchi moja ikiwekewa vikwazo na nyingine ikitaka kusaidia nayo inawekewa.

"SADC mmeanzisha (suala la Zimbabwe) muichukue muipeleke AU (Umoja Afrika)," alisema.

Mtoa mada, Prof. Gordius Kahyarara, akijibu swali lililotaka kujua kama vikwazo wamewekewa viongozi na chama kwa nini ionekane ni tatizo, alisema vimewekwa kitaalam na madhara yake ni Wazimbabwe.

Mtoa mada mwingine, Dk. Godfrey Sansa, alisema hawawezi kuishinda vita hiyo kama wataendelea kwenye upotofu wa fikra.

"Kitu cha kwanza ili tuwe na fikra pevu, vyuo vikuu visiingizwe au vinusurishwe na fungate la kisiasa, tusiruhusu masuala ya kisiasa yakawa sehemu ya wasomi wetu, kwa sababu mgawanyo tunaousema hapa hata viongozi tuwafundishe.

"Mnataka kila chama kiwe na chuo, hapana vyuo vyetu viwe huru kwa kila mtu wa itikadi ya kidini yeyote, tumfundishe atakapokwenda kokote atakuwa kiongozi bora, tuache kufanya makundi ya vyama kwenye vyuo vikuu.

"Sipepesi macho kwenye hili atakayechukia anichukie kwa sababu hata Mwalimu (Baba wa Taifa, Julius Nyerere) hakufanya hivyo, hivi sasa vyuoni unakuta hawa ni wa chama fulani, hawa wanafunzi ni viongozi wa chama fulani, sisi wote ni Watanzania kwenye chuo ni wanataaluma." alisema.

Jambo la pili aliiomba SADC kwa kueleza kuwa akisoma mikataba haoni kama kuna sehemu imeelezwa wazi, majukumu ya taasisi za elimu ya juu kwenye mapambano dhidi ya vikwazo vya kibeberu.

"Sisi ndio tunaambiwa tuwaeleze watawala nini cha kufanya siyo tuwasikilize wao watueleze nini cha kufanya, Mwalimu alisema wazi vyuoni ni mahali pa kufikiri kwa uhuru, hebu tupafanye kweli kuwe mahali pa kukuza fikra pevu za kufikiri," alisema.

Mtoa mada mwingine, Dk. John Jingu, alisema vikwazo vya kiuchumi ni nyenzo katika vita za uchumi na vina madhara makubwa katika maisha ya wananchi kuliko vita vingine.



Mkazi wa bonde la Yaeda Chini, wilayani Mbulu, Gidamuda Gidalika akizungumzia changamoto ya maji na zahanati kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vijana wapatiwa mafunzo ya ujasiriamali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Arusha Municipal Community (AMCF) kwa kushirikiana na Foundation for Civil Society (FCS), kupitia mradi wa majukwaa ya vijana, imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 28,000 wa kata tatu za halmashauri ya Jiji la Arusha ili kuwajengea uwezo wa kupambana na umaskini.

Akizungumza juzi wakati wa mashindano ya maonyesho ya bidhaa kutoka kwa vijana hao, Ofisa Tawala Msaidizi wa AMCF, Anna Mushi, alisema mafunzo hayo yametolewa kupitia majukwaa mbalimbali ya vijana wa kata za Lemara, Unga Limited na Sokoni One.

Mushi alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia vijana kiuchumi kwa kuwafundisha njia za uhakika za kuzalisha bidhaa bora ili kujiajiri.

Alisema mradi huo unawakusanya vijana kwa pamoja katika kata hizo kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uongozi, utawala bora, kushiriki katika shughuli za kiserikali kwa ajili ya maendeleo, kutambua fursa zilizopo kwenye jamii na kushiriki katika ngazi za kutoa uamuzi.

Aliongeza kuwa kupitia mradi huo, wametoa elimu kwa vijana juu ya ujasiriamali na masoko, biashara na ubunifu ili kukuza na kuongeza kipato.

"Tunawahamasisha vijana hapa nchini kuwa wajasiriamali wasitegemee kuajiriwa tu hususan wale walioko vyuoni. Tuzingatie sera ya serikali kuwa nchi ya viwanda na tunawashauri kujiunga katika makundi mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhani, alisema katika bajeti ya mwaka 2018/19, halmashauri hiyo ilitoa mikopo ya Sh. milioni 665 kwa vikundi 118 kutoka kata 25 za jiji.

Alisema maelekezo ya serikali kila mwaka wa bajeti, halmashauri zote nchini zimetakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Muongozo wa serikali unasema asilimia kumi ya mapato yaliyokusanywa na halmashauri zote nchini asilimia 10 zigawiwe kwenye vikundi vya vijana, wanawake watu wenye ulemavu,"alisema Hanifa.

Wakizungumza kwa niaba ya vijana wengine walioshiriki maonyesho hayo, Ibrahim Kikoti na Sara Moses , walisema kupitia mafunzo hayo, yamewaongeza maarifa ya kuwa wabunifu wa kuchangamkia fursa kwa kuzalisha bidhaa bora na kutafuta masoko ya uhakika.

"Kilichosababisha mimi kuingia katika ujasiriamalia ni mafanikio na maendeleo yanakuja kwa kasi. Watu wanapochukua jukumu la kujiajiri inawasaidia kukuza kipato kwa kuwa kazi anayoifanya ni yake, hivyo ataweza kuimudu kwa njia yoyote," alisema Moses.

Aliongeza kuwa vijana wengi wamekuwa wakilalamika kuwa ajira zimekuwa chache na hazipatikani kwa urahisi. Suala hilo linatokana na vijana wengi kutokujishughulisha na kazi, sambamba na kutokuwa na ubunifu wa kutumia fursa zilizopo.

## Watoto 272,600 kuchanjwa surua

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

WATOTO 272,633 wenye umri wa miezi tisa hadi miezi 59 walio chini ya miaka mitano, wanatarajia kupata chanjo ya surua-rubella na polio kwenye mkoani Manyara.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, aliyasema hayo juzi, akizungumza wakati wa uzinduzi wa chanjo hiyo inavyoendelea mkoani humo, tangu Oktoba 17, mwaka huu.

Dk. Kayera alisema chanjo hiyo ni kampeni ya kitaifa ya kuzuia na kupambana na magonjwa yanayozuilika na kuongeza kinga kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema huduma za chanjo hizo, zinapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na maeneo yaliyopendekezwa ya karibu na makazi ya wananchi.

"Kinachofanyika hapa ni kutoa chanjo pekee, hayo yanayozungumzwa kuwa kutakuwa na ugawaji wa chandarua siyo kwenye shughuli hii ya chanjo ya surua- rubella," alisema Dk. Kayera.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Jesca Lebba, alisema watoto 36,000 wanatarajiwa kupata chanjo ya surua-rubella katika wilaya yake.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Babati, Dk. Hosea Madama, alisema katika wilaya hiyo, watoto 56,8600 wanatarajia kupata chanjo hiyo.

Wilayani Kiteto, Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Malkiadi Mbota, alisema watoto 48,000 wanatarajiwa kupata chanjo ya Surua-Rubella katika wilaya hiyo.

Utolewaji wa chanjo hiyo ni kampeni ya nchi nzima na Mikoa yote ilianza kutoa huduma hiyo, tangu Oktoba 17, mwaka huu.

# Wahimizwa kuwapa watoto lishe bora

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZAZI wameshauriwa kuwapatia vyakula vya aina mbalimbali watoto wao wenye umri chini ya miaka minane na kuviandaa vizuri ili wakue katika afya bora.

Rai hiyo ilitolewa jana mjini HAPA na Dk. Anna Akaro, kutoka kitengo cha watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara wakati akizungumza na Nipashe juu ya madhara ya ulaji ovyo kwa watoto.

"Mtoto anapohitaji kula chakula usimnyime maana watoto hawana muda kamili wa kula kwa kuwa mtoto anaweza akala kidogo akakimbia kwenda kucheza, hivyo akirudi akitaka kula mzazi ampe ili mradi chakula kiwe 'fresh'," alisema.

Dk. Akaro alisema watoto wanapobadilishiwa vyakula na kuandaliwa vizuri na kupewa kwa wakati, kunaimarisha afya za watoto na hakuna madhara yatakayowapata kwa kuwapa vyakula hivyo.

Aidha, alisema watoto wakipewa chakula kila mara ni ruksa ila ni vizuri kuepuka kuwapatia vyakula vya sukari zaidi ili kuwaepusha madhara ya meno kuumia.


"Vyakula vya sukari havifai kuwapa watoto, sababu wataumia meno yao,hivyo vema wazazi wakaepuka kuwapa watoto vyakula hivi," alisema.

"Ukiwapa matunda , mayai, machungwa ni vizuri zaidi maana vinamjenga kwa ukuaji na ukimbadilishia chakula badilisha hata mboga watafurahi zaidi," aliongeza.

Mmoja wa wazazi, Imelda Alphonce, alisema katika suala la kuwapatia watoto vyakula kila wakati, kunahitajika elimu kwa wazazi ili jamii ijue na kuchukua hatua kwa ajili ya kuokoa watoto.

Mkazi wa Mtaa wa Negamsi, Godwin Zephania, alisema shida ya wazazi wengine wanawadekeza watoto kwa kuwanunulia vitu vyenye sukari kama pipi au biskuti kila mara, hivyo kuwaathiri watoto meno, na kuwataka kuepuka kuwapa vitu hivyo kila wakati.

"Wazazi wanaona upendo lakini wengi hatujuwi kwamba kuwapa watoto vitu vitamu kila wakati tunawasababishia watoto madhara ya baadaye,"alisema.



# DC awapa rungu kusaka wahalifu

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amewapa mgambo idhini ya kutafuta maficho ya wafanyabiashara wa mihadarati na gongo wilayani Hai ili kuwasaidia polisi kushughulikia uhalifu.

Aliwapa rungu wakati alipokutana nao katika kikao cha kazi kwenye viwanja vya halmashauri ya wilaya hiyo.

"Mgambo shirikianeni na Jeshi la Polisi, anzeni mara moja operesheni za mara kwa mara zitakazowezesha kutambua maeneo yote yanayohusika na uuzaji wa dawa za kulevya pamoja na utengenezaji wa pombe haramu aina gongo ndani ya wilaya yetu, hicho ni kibali rasmi nimewapa,"aliagiza

Katika kikao hicho, Ole Sabaya alisema hivi sasa ni wajibu wao kuhakikisha wanafanya opereshini hiyo ambayo pia itasaidia kujua, kutambua wageni wote wanaoingia wilayani hapo na shughuli wanazozifanya.

Alitaka askari hao kwa kufuata muongozo watakaopewa na Polisi Kata, kwa kuwa lengo la serikali wilayani humo ni kuhakikisha kuwa Hai inakuwa salama na kupunguza uhalifu.

Pia aliwatahadharisha asitokee mgambo akajaribu kumuonea mtu wakati wa oparesheni hiyo, huku pia akiwaasa kutokujiingiza katika biashara ya uuzaji wa dawa za kulevya pamoja na pombe haramu ya gongo na atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kisheria.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya Upendo Wela, aliwataka askari hao kuwa na uzalendo wakati wa utekelezaji wa operesheni hiyo, nidhamu na kuzingatia kiapo walichokiapa ili kuwetekeleza majukumu yao kikamilifu.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Elia Machange alisema halmashauri itashirikiana na jeshi hilo wakati wote.

Mkurugenzi huyo alilipongeza jeshi hilo kwa kuchangia kuwapo amani kwa wakati wote ndani ya wilaya hiyo.

# Wananchi wasalimisha 700,000/- fedha bandia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

BAADHI ya wananchi wilayani Hai wameitikia wito wa Mkuu wa Wilaya, Lengai Ole Sabaya, wa kurudisha noti bandia kwenye vyombo vya dola na kusalimisha takribani noti feki zenye thamani ya Sh. 740,000.

iki hii Sabaya alitoa saa 72 za kuwataka wenye noti bandia popote kuzisalimisha ofisini kwake au kituo kikuu cha polisi Bomang'ombe kuepuka kwenda jela,

kuu wa Wilaya jana alithibitisha kupokea fedha hizo kutoka kwa baadhi ya wananchi walioitikia msamaha alioutoa siku nne zilizopita mbele ya maofisa wa Benki Kuu ya (BoT), Kanda ya Arusha.

Ni kweli baada ya kufanya mkutano na BoT pamoja na zaidi ya wananchi 850, nilitoa siku tatu nikasema yeyote atakayesalimisha fedha hizo za bandia, baada ya kuonyeshwa tofauti ya fedha halali na bandia ni ipi, mpaka sasa tumeshapokea Sh. 740,000," alisema Sabaya.

"Na nimesema baada ya siku tatu nilizotoa kumalizika, tukikukuta na fedha bandia utatuonyesha zilipotengenezwa na huo utakuwa msalaba wako mwenyewe."

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, wahalifu wanaosambaza fedha hizo wanabadilisha Sh. milioni moja bandia kwa Sh. 250, 000 hadi 300, 000 halali. Mwanzoni mwa wiki hii, Benki Kuu ya Tanzania ilikiri kuwa tukio la kukamatwa kwa noti bandia zinazofikia Sh.milioni 11 katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wanaona kwamba hali hiyo inaanza kujirudia kama ilivyokuwa zamani. Akizungumza na wananchi wa Hai katika mkutano wa kutoa elimu, Meneja Msaidizi wa Kitengo cha Sarafu wa Benki Kuu, Kanda ya Arusha, Robert Mathew, alisema kwa Mkoa wa Kilimanjaro kwa sasa hivi ni mara ya kwanza kujitokeza kwa taarifa hizo.

Meneja huyo alisema mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambayo ni Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara mzunguko wa pesa bandia umepungua.

"Lakini hili tatizo ambalo limetokea Wilaya ya Hai, tunaona kwamba hali inaelekea kujirudia kama mwanzo, hata hivyo suala lipo mikononi mwa Polisi na wao watafanya uchunguzi na watajua chanzo ni nini, sisi tuko upande wa kutoa elimu tu kusudi wananchi wasije wakaingia kwenye kupata hasara.

Kwa mujibu wa BoT, hali hiyo ikiachwa bila kutoa elimu inaweza kusababisha mtu binafsi uchumi wake ukaharibika, vile vile hata upande wa serikali ni hasara, kwa kuwa kitakuwa kimeingia kitu katika mzunguko ambacho hakipo kwenye mpangilio, maana yake ni lazima uchumi uharibike.

Alisisitiza elimu kuwa umakini wa vyombo vya usalama kudhibiti vitendo vya uhalifu na elimu ya uhamasishaji vimechangia kuleta matokeo chanya yanayosaidia kukuza uchumi.



Sehemu ya mawakala wa utalii kutoka nchi mbalimbali duniani, wakiwa wameshikana mikono ili kucheza ngoma ya Wachaga kama sehemu ya kujifunza utamaduni, wakati wa kuandaa kahawa kwa njia ya asili, uliofanyika Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro jana.
**PICHA: ASRAJ MVUNGI**

# Halmashauri kuhamia kwenye majengo yake

**Na Godfrey Mushi**, MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Moshi, imetangaza rasmi kuhamia kwenye majengo yake ifikapo Novemba 5, mwaka huu.

Kastori Msigalla, Mkurugenzi wa Halmashauri alitangaza katika kikao cha Menejimenti ya Halmashauri (CMT) kwamba ofisi hiyo bila kusukumwa Novemba 5 mwaka huu.

"Wakuu wote wa idara muandae watu wenu kwa hili, tutahama tarehe 5 mwezi wa 11 kuelekea Kolila katika Kijiji cha Kikarara. Tunatarajia kwamba ofisi yetu kuu ya wilaya itahamia Kata ya Old Moshi Mashariki, kwenye majengo ya iliyowahi kuwa Shule ya Sekondari Kolila, hakuna mjadala ni kuhama tu,"alisisitiza Msigalla

Kwa mujibu wa Msigala, kuna gharama za kuhamia eneo hilo ukilinganisha na gharama za kuhamia eneo la Mji Mdogo wa Himo, uliopo Njiapanda ya barabara ya Moshi/Dar es Salaam.

Hatua hiyo inakuja baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kutangaza agizo hilo la Rais John Magufuli, Oktoba 7 mwaka huu wa kuzitaka halmashauri kuhamia kwenye majengo yao. Baada ya agizo hilo baadhi ya wanasiasa walianza chokochoko za kupingana na agizo hilo, wakitaka ofisi za Halmashauri ya Moshi zihamie eneo jingine badala ya Kolila.

Katika maelekezo yake, Msigalla alisema "Sisi ni watumishi wa umma tupo tayari kuwahudumia wananchi wetu kwa kiwango chetu kile kile cha ubora kwa hali yoyote katika kuhakikisha tunatimiza wajibu." Aidha, Mkurugenzi alitoa baraka kwa viongozi na watumishi wa Halmashauri ya Moshi kutembelea eneo la makazi mapya ya ofisi za makao makuu ya Halmashauri ya Moshi ili kujiandaa na kuweka mazingira rafiki yatakayowezesha kutoa huduma kwa wananchi.

Shule ya Sekondari Kolila ambayo awali, ilikuwa ikimilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, ilifungwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kutokana na kushindwa kujiendesha.

Uamuzi huo wa Halmashauri ya Moshi, kutengeneza historia mpya ya kupeleka ofisi zake ukanda huo wa juu wa milimani, iliridhiwa na Baraza la Madiwani, baada ya Mwenyekiti wa Michael Kilawila, kutangaza uamuzi ulioridhiwa na kikao cha dharura cha baraza hilo.

Hata hivyo mpango huo ulipingwa na wanasiasa wachache waliokuwa wakitengeneza visingizio na chokochoko za kutaka wananchi wapinge Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuhamia katika majengo ya iliyokuwa Sekondari Kolila.

Wapingaji walikuwa wakitengeneza vikwazo ili kuwashawishi baadhi ya wananchi waamini kwamba Kolila ambako halmashauri hiyo inahamishiwa ni mbali







Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha nyara ya serikali jino la Tembo, jijini humo jana, lililokamatwa na jeshi hilo, katika Kijiji cha Mkoka, Wilaya ya Kongwa, mkoani humo juzi, likiwa limehifadhiwa kwenye mfuko wa salfeti ambapo watuhumiwa wawili wanashikiliwa kwa kukutwa na nyara hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watamani mbinu mpya kudhibiti ukatili kijinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto vikiwamo vitendo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto wa kiume, wametakiwa kuibua mikakati mipya itakayosaidia kuwatia hatiani watuhumiwa wa matendo hayo.

Rai hiyo ilitolewa jana na mratibu wa mradi wa tuwalinde kutoka shirika linalojihusisha na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsi la (Ajiso) mkoani Kilimanajaro, Tatu Mrutu wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kwenye mkutano ulioandaliwa na TGNP Mtandao.

Mrutu alisema kuwa hivi sasa watuhumiwa wa vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa wale wanaobaka au kulawiti watoto wamekuwa na uwezo mkubwa wa kuharibu ushahidi.

Alisema hivi sasa watuhumiwa wanaobaka watoto wamekuwa makini kwani mara baada ya kufanya vitendo hivyo wamekuwa wakiwaogesha ili kuharibu ushahidi.

Aidha, alisema mikakati hiyo mipya itawezesha kuongeza mbinu za kuwakamata watuhumiwa wa ubakaji katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Aidha, aliwaambia kuwa vitendo vya ukatili vimekuwa vikichangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo mila na destri potofu katika jamii. "Unakuta wakati fulani mtu anaweza kwenda kwa mganga akaambiwa ili uwe tajiri unatakiwa kufanya ngono na mtoto wa dada yako ambaye ni bikira ndipo mambo kama haya yanatokea"alisema Mrutu. Alieleza kuwa sababu nyingine ni wazazi kutengana ambapo mama anabaki na watoto pekee yake na kushindwa kuwasimamia hivyo kujikuta wakiishi na kufanya maamuzi yao wao wenyewe.

"Lakini pia zipo sababu za kisiasa ambapo wanasiasa wamekuwa wagumu kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kutokana na wengi wao kuhofia kupoteza kura zao hivyo kuuficha ukweli wakati fulani sisi kama shirika tulikutana kesi ya diwani kubaka mtoto lakini ilifichwa taarifa ile"alisema

Naye ofisa utafiti na uchambuzi kutoka TGNP mtandao, Zainabu Mmari, alisema kuwa lengo na mkutano huo ni kuyakutanisha kwa pamoja mashirika ambayo yamekuwa yakitekeleza miradi ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na The Foundation For Civil Society (FCS).

Mmari alisema katika mkutano huo jumla ya mashirika 29 yameshiriki kutoka katika mikoa mbalimbali bara na visiwani na TGNP ndiyo waratibu wakuu katika utekelezaji wa miradi yote.

Alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu na kubaini changamoto pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye kutekeleza miradi katika mashirika hayo.

Alisema moja ya changamoto iliyopo katika maeneo mengi ni rushwa pamoja na hali ya maeneo kutofikika ambapo watoto wanaobakwa wamekuwa wanashindwa kufika katika vituo vya afya kufanyiwa vipimo ndani ya saa 48.

# Shule yakabidhiwa kifaa kudhibiti utoro

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ILI kudhibiti utoro kwa wanafunzi na kuboresha mahudhurio ya vipindi darasani, Shule ya Sekondari Dodoma, imekabidhiwa kifaa cha kudhibiti mahudhurio.

Kifaa hicho ni ' biometric time attendence' chenye uwezo wa kuangalia watu 500,000 na mdau wa kuendeleza elimu kampuni ya G.Tech ya Dodoma.

Kifaa hicho kimetolewa na kampuni hiyo baada ya uongozi wa shule hiyo kuomba msaada huo kwani shule hiyo haina uzio na ipo katikati ya jiji la Dodoma.

Akizungumza katika mahafali ya kidato cha nne jana mara baada ya kukabidhiwa kifaa hicho chenye uwezo wa kuangalia watu 500,000 Mkuu wa Shule ya Dodoma, Aman Mfaume, alisema kifaa hicho kitawasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti utoro wa wanafunzi na kuboresha mahudhurio.

Alisema awali ilikuwa vigumu kudhibiti wanafunzi wote kwa sababu hakuna uzio, kwa hivyo inapofika muda wa mapunziko Mwanafunzi anaweza kutoroka vipindi au kuchelewa paredi shuleni na kuingia kupitia njia za panya.

"Nawashukuru sana kampuni ya G.Tech kwa sababu wakati tukisubiri kukamilisha taratibu za kujenga uzio, kifaa hiki kitatusaidia kuzuia utoro kwa wanafunzi kwa sababu ni lazima usaini muda wa kuingia na kutoka unatakiwa usaini," alisema Mfaume.

Aliwaambia kuwa anaamini kifaa hicho kitakuwa msaada mkubwa kwao kudhibiti hayo yote na mahudhurio yataimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na kwamba hawana ujanja wa kukwepa darasani.

Mbali na hilo alisema hata walimu pamoja na kuwa na kitabu cha kusaini nao watalazimika kukitumia kwa sababu kina uwezo wa kuangalia idadi ya watu wengi ambapo shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1,352 wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Aidha, alisema zinahitajika Sh. milion 263 ili ujenzi wa uzio huo ukamilike ambapo wameanza kufanya harambee kwa wadau ili kuhakikisha wanapata fedha hizo.

Meneja wa kampuni ya G.Tech tawi la Dodoma Elirehema Msuya, alisema kifaa hicho kina uwezo wa kuonyesha sura ya mwanafunzi aliyesaini muda wa kuingia na kutoka.

"Biometric Time Attendance ni kifaa muhimu sana kuwa nacho kinasaidia kudhibiti utoro shuleni na ofisini kwani ni vigumu wanafunzi kutoroka," alisema Msuya.

Mgeni rasmi katika mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo mbunge wa vijana Mkoa wa Dodoma, Mariamu Ditopile, aliwataka wanafunzi hao kuzingatia elimu kwa sababu ndio kila kitu.

# 'Zielekezeni nguvu mimba za utotoni'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Spika, Dk Tulia Ackson, amewataka Watanzania pamoja na wadau mbalimbali kutobweteka na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Rufani juu ya umri wa kuolewa wa kuanzia miaka 18.

Aidha, amewataka badala ya kuendelea na mijadala hiyo wajikite kwenye mapambano ya mimba za utotoni.

Tulia aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa halmashauri kuu ya Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania nchini (Umati).

" Umati mjipange vyema muitumie hii hukumu kupeleka elimu kwa jamii kwasababu hii hukumu haitaweza kwenda kichwani mwa mtu kama vile wote mnavyopenda, tungependa watu wenye miaka 18 ndiyo waanze kufikiri ndoa lakini sote tunafahamu hata miaka 18 si kwamba wako tayari kwa ajili ya ndoa,"alionya.

Alisema miaka 18 bado ni midogo kuanza kufikiri kuhusu kulea familia na kuwataka Watanzania kutoa elimu zaidi ili vijana wenye umri mdogo wajitambue na hivyo kufanya maamuzi sahihi.

Aidha Dk.Tulia alisema kuwa serikali itaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na chama hicho cha Umati nchini katika masuala ya afya nchini.

"Endeleni kupeleka elimu kwa jamii juu ya masuala ya afya ya uzazi pamoja na ujinsia kwani hivi sasa serikali imejenga vituo vya afya kote nchini hivyo wajibu wenu kuwahamasisha wanachi kuvitumia katika kupata huduma mbalimbali za fya"alisema

Mwenyekiti wa Umati Taifa, Jasmeen Massengi, alisema miongoni mwa mafanikio waliyoyapata katika miaka 60 tangu kuanzishwa kwao ni kuwawezesha wasichana walio nje ya shule na katika mafunzo ya ufundi na kuongeza uelewa wa sheria na kanuni za kuwalinda watoto.

Juzi Mahakama ya Rufani ilitupa rufani ya serikali dhidi ya hukumu ya Mahakama Kuu iliyobatilisha vifungu vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto wa kike chini ya miaka 18 kuolewa.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia), akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China (CCP), Guo Yezhou (kushoto), wakati alipofika Ikulu mjini Zanzibar jana, akiwa na ujumbe wake. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wajasiriamali wa kahawa wafunzwa mbinu mpya

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda, imewataka wajasiriamali kujifunza mbinu bora za kuandaa kahawa ili kukidhi mahitaji ya wanywaji wa kinywaji hicho.

Kwa kufanya hivyo wajasiriamali wataongeza wigo na kupanua fursa za ajira na biashara ndani na nje ya nchi.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Khadija Khamis Rajab, wakati akifungua mafunzo maalum kwa wauza kahawa wa Zanzibar.

Aliwaambia mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa kwa ajili ya kuongeza ujuzi katika biashara ya kahawa ambayo inafanywa na wajasiriamali wengi wa visiwani Zanzibar.

Alisema wajasiriamali wengi wanaojishughulisha na biashra ya uuzaji wa kahawa hawana ujuzi wa kupika kahawa inayovuta wateja na ile iliyoshauriwa na wataalamu wa afya hivyo fursa ya mafunzo hayo ni kusaidia kuleta mbinu ya kuboresha biashara zao.

Aliwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo waliyoipata ili kutengeneza kahawa bora ambayo itavuta wengi na kupanua wigo wa biashara zao ndani na nje ya Zanzibar.

"Zanzibar kahawa inatumika sana na tuna hoteli za kitalii pia ambazo hutumia kahawa kwa hivyo mafunzo haya yatasaidia hata kuboresha kahawa zenu mnazotengeneza hivi sasa na kuwa bora na zenye viwango vinavyotakiwa," alisema

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo Biashara Tanzania (Tantrade) Latifa Khamis, alisema pamoja na faida lukuki za kinywaji cha kahawa ambacho kimeelezwa na wataalam wa bodi ya kahawa, matumizi ya ndani ya nchi kwa ujumla wake ni kidogo sana Alisema wastani asilimia nane ya kahawa inayozalishwa nchini ndiyo inayotumika nchini na asilimia 92 kusafirishwa kwenda nje ya nchi hasa nchi za Ulaya, Japan na Amerika. Aliongeza kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa katika kutangaza unywaji wa kahawa bado Watanzania wengi hawafahamu kwa usahihi faida za unywaji kahawa .

Hivyo alitoa wito kwa Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na Tantrade pamoja na Wizara ya Biashara na Viwanda kuandaa mfumo rasmi wa upatikanaji wa bidhaa hiyo na kuvirasimisha vituo vya uuzaji wa kahawa hapa Zanzibar.

Kaimu Mkurugenzi wa Ubora na Uhamisishaji Bodi ya Kahawa Tanzania, Frank Nyerusi, alisema duniani biashara kubwa baada ya mafuta ni kahawa na kwamba vikombe 3,000,000 hunywewa kila mwezi. Alisema mafunzo hayo yalifikiwa baada ya kugundua unywaji wa kahawa unaimarisha afya na husafisha figo.

# SMZ kufuatilia shule binafsi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), itaendelea kuzifuatilia shule binafsi kwa lengo la kufuatilia ubora wa elimu inayotolewa. Akizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne wa shule ya Feza Zanzibar, Said alisema shule zote za Zanzibar zinatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa ili kuhakikisha kunakuwa na usawa katika utoaji wa elimu. Alisema Wizara ya Elimu, imeweka miongozo na sheria mbalimbali za utoaji wa elimu shuleni bila kujali ni za serikali au za binafsi, ambayo huifuatilia ipasavyo ili kwenda sambamba katika utoaji wa elimu bora kwa wote. Alisema Wizara itaendelea kushirikiana na shule binafsi ili kuimarisha elimu Zanzibar na kufikia ufaulu bora.

Said alisema amefarajika kuona kuwa Feza Zanzibar, ni shule inayotii na inatekeleza miongozo yote iliyotolewa na Wizara. Aidha, aliwataka wanafunzi wa kidatu cha nne kuhakikisha wanafuatilia zaidi masomo yao pamoja kutumia vizuri simu na mitandao ya kijamii kwa kujifunza tu na sio kwenye masuala maovu.

Naibu Waziri wa Elimu kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, aliwatakia heri na mafanikio wanafunzi wote wa wanaotarajiwa kuanza mitihani yao ya kidato cha nne November 4, mwaka huu.

# Apongeza umahiri wa sera ya elimu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema kuwapo kwa sera bora ya elimu nchini kunawatengenezea mazingira mazuri ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi.

Ayoub aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na walimu na wanafunzi wa shule ya Kibele wakati wa mahafali ya mafunzo maalumu ya kujifunza lugha ya Kingereza yaliyofanyika katika shule hiyo.

Alisema kuwa kumekuwa na baadhi ya watu wanatabia ya kubeza jitihada za serikali katika kuleta maendeleo kwa kuikosoa sera ya elimu ya nchini bila ya kufanya uchunguzi wa hoja zao.

Aidha , Mahmoud alisema Serikali ya Mapindunzi ya Zanzibar, huzifanyia marekebisho mara kwa mara sera mbali mbali kutokana na mahitaji yaliyopo na muda ili kukidhi malengo yaliyokusudiwa.

Aliongeza kuwa Sera ya Elimu ya Zanzibar ni andiko lililo imara katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuwa inawajali wananchi wake kielimu , hivyo kila mara huifanyiya marekebisho kuendana na wakati huku serikali ikijitahidi kuboresha miundombinu ya elimu kwa kutoa elimu bila ya malipo.

"Si vyema kuinyooshea vindole Sera ya Elimu ya Zanzibar kuwa haina ubora kwani tangu kuazishwa kwa sera hiyo imeleta mafanikio makubwa kwa kuwasongezea wananchi huduma ya elimu karibu, kufuta tozo kwa wanafunzi sambamba na kuweka miundo mbinu imara," alisema Mahmoud.

Aliwataka walezi na wazazi pamoja na walimu kushirikiana na serikali katika kuhakikisha vijana wa Mkoa wa Kusini wanajihusisha na kusaka elimu na kuachana na mila zisizo sahihi pamoja kuwataka wanafunzi kujua wajibu wao wa kujipatia elimu.

Mapema Mkuu wa Wilaya ya Kati Hamida Mussa Khamis, aliwahimiza wazazi na walezi kujali jitihada za Serikali ya Mapindunzi Zanzibar kwa kuwapatia vijana elimu bure na iliyo bora na si vyema kudharau jitihada hizo kwa kuwafanyisha kazi muda wa masomo.

Alisema serikali ya mkoa inafanya uchunguzi juu ya changamoto iliyotolewa na wanafunzi inayo inayosababisha kufeli ya kutojua Kingereza ili kuipatia ufumbuzi wa haraka.

Mwalimu Mustafa Shaffi Khatibu, alieleza mafanikio walioyapata tangu kuazishwa kwa darasa hilo maalumu la Kingereza kwa lengo la kuandaa vijaana walio imara na wenye uwezo wa kujiamini katika kukabiliana na mitihani ya taifa.

Akisoma risala ya wanafunzi wa darasa maalumu la Kiingera, Khadija Mussa Ali, alisema tangu kuazishwa kwa darasa hilo kuna mabadiliko mbalimbali walioyapata ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo wa kuzungumza licha ya kuwapo kwa baadhi ya changamoto na kumuomba Mkuu wa Mkoa wa Kusini kuwatatulia matatizo hayo. Darasa hilo maalum la kujifunza Kiingereza lina wanafunzi 36 na ni mahafali ya sita tangu kuanzishwa kwake.



**HARMONIZE** Soma UK.14

JUMAMOSI OKTOBA 26, 2019

BT
BURUDANI
TELE



# VANESSA WEWE!

## AJIRUSHA KWEUPE NA MNIGERIA

Soma UK.16

## BASI SAWA




## Ali Kiba umezaliwa na nyota yako

MFALME wa muziki wa Bongo fleva, Ali kiba, ametunukiwa nafasi ya ubalozi wa utalii wa Zanzibar.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mahmoud Kombo, alimkabidhi cheti cha kumtambua mwanamuziki huyo kabla ya kuanza kazi yake rasmi.

"Nina furaha kubwa kutunukiwa Cheti cha ubalozi wa Utalii wa ndani ili kuongeza chachu zaidi katika kukuza utalii wa Zanzibar na Tanzania kiujumla, kwa Watanzania wenzangu na hata watalii kutoka nchi mbalimbali, tunaendelea kuwakaribisha" alisema Kiba.



## Harmonize kafunguliwa, mwache aseme

MKALI wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, ambaye anatamba na wimbo wake mpya unaoitwa 'Uno' ameshambulia vyombo vya habari kuwa vinachangia kuua vipaji vya baadhi ya wasanii.

Akizungumza katika redio moja hivi karibuni, Harmonize amesema kuwa tofauti za kibiashara zilizopo kwenye vyombo hivyo inaua muziki wa Bongo Fleva kwa kuwa zinawagawa wasanii.

"Katika kitu kinachorudisha chini muziki wetu ni tena kwa kasi sana, Ni ugomvi baina ya Media kwa Media. Kwa sababu sasa hivi msanii kabla hajatoka anawaza niende upande gani? akienda huku atabaniwa, Akienda huku atabaniwa. Kuna wasanii wengi wazuri wametoka lakini wanaishi mazingira magumu sana, inatakiwa tukae chini na tuyamalize"amesema Harmonize na kuwatolea mfano Marioo na Whozu.



# LIL OMMY AING'ARISHA TANZANIA

WIKI hii Tanzania imepata taarifa nzuri kutoka New Jersey nchini Marekani, baada ya mtangazaji wa radio Times FM, Omary Tambwe maarufu kama Lil Ommy, kushinda tuzo ya African Entertainment Awards (AEAUSA).

Lil Ommy ambaye anaendesha kipindi cha 'The Playlist' kinachofanya mahojiano maalum na watu maarufu alishinda kipengele cha Mtangazi Bora Afrika.

Waandaaji wa tuzo hizo zilizofanyika kwa mara ya tano walilitaja jina la Lil Ommy kwenye kipengele kilichopewa jina la 'Best Host', na kuwatupa chini watangazaji wengine tisa kutoka Afrika.

Mtangazaji huyo ametumia mtandao wa Twitter kuwashukuru mashabiki wake kwa kumuunga mkono na kumpigia kura.

"Asante sana kila mmoja kwa kura zenu na sapoti yenu ya kutosha, ASANTE SANA MASHABIKI wooote kwa kura na nguvu yenu imeonekana... Love always win.... Tumeweza kuichukua tuzo ya Mtangazaji Bora wa Mwaka Afrika," Lil Ommy ametweet.

Mwaka huu, Lil Ommy alitajwa kuwania tuzo tatu kubwa za kimataifa kama Mtangazaji Bora.

Ameshinda tuzo ya kwanza ya AEAUSA, lakini pia anasubiri Tuzo za AFRIMMA zitakazofanyika leo huko Dallas nchini Marekani.

Katika tuzo hizo kwenye tasnia ya habari pia kutoka Tanzania DJ D Ommy wa Clouds Fm atakuwa Mtanzania pekee anayewania tuzo ya DJ Bora Afrika.

Usiku wa leo pia Lil Ommy atakuwa akiwania Tuzo ya Mtangazaji Bora kwenye 'Tuzo za StarQT' zitakazotolewa nchini Afrika Kusini.

## INSTA-TWITTER





**Nipo** benki. Kuna dada ametukana foleni wote na kwenda kukaa mbele. Nashangaa wanaolalamika kukatwa foleni wote ni wanawake. Wababa tumepiga kimya-**Idriss Sultan.**



**Pengine** utashuhudia mateso mengi kwenye safari ya maisha yangu. Lakini nakuhakikishia nitayashida yote na kuwa mpya mwenye furaha, mafanikio na kuhakikisha nalifikia kusudi la aliyeniumba-**Elizabeth Michael Lulu.**



## Gari la Hamisa laibua mjadala mkali

GARI la Mwanamitindo na Msanii wa Muziki, Hamisa Mobetto, ambalo amemzawadia mama yake limezidi kuibua mijadala katika mitandao ya kijamii.

Wiki hii kwenye ukurasa wa mama yake Hamisa (Mama Mobetto) aliandika "Alhamdulilaah kwa kila jambo mwanangu Allah akuongezee zaidi na zaidi ulipotoa Allah akupe kikubwa zaidi nakupenda sana nakuombea siku zote."

Hamisa limjibu mama yake kwa kusema anampenda sana na angekuwa na uwezo angempa Dunia.

Baada ya posi hizo, wadau wa mitandao waliamza kujadili gari hilo huku wengine wakimpongeza kwa hatua yake hiyo na baadhi walionesha kuwa na wasiwasi kama na uhalisia wa jambo hilo.




@burudanitele

>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow



## UMEMSIKIA MKE WA NKURUNZIZA AKIIMBA?

UMEMSIKIA mke wa rais wa nchi akiimba? Basi kutana na mama Denise Nkurunziza, mke wa kiongozi wa Burundi ambaye ametoa singo kali ya wimbo unaokemea unyanyasaji wa wanawake.

Video wa wimbo huo unaanza kwa picha ya mwanamke anayemkaribisha mume wake nyumbani na kumkaribisha kula chakula cha jioni ambaye anamtemea mate ghafla na kumpiga.

"Hauna maana katika nyumba hii ,tumbo lako kila wakati limejaa maharage, huku matumbo ya wanawake wengine yamejaa watoto wachanga."

Bi Nkurunziza, mwenye umri wa miaka 49, alisikika mwenyewe akitoa ushauri wa maridhiano, akielezea kwamba "Suala la kutokuwa na uwezo wa kuzaa linaweza kutokea kwa mwanamke au mwanamke ".

Nkurunziza na mkewe wana watoto watano pamoja na kuwaasili wengine kadhaa.

## INSTA-TWITTER




Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Maisha** hayataki mapepe. Jipange- **Shetta.**



**Yaani** Unai (Kocha wa Arsenal), acha nikaoge na kitaulo changu-**Madee Ali**.



**Ni** rahisi kuona mtu anaekimbia kwenye kundi la watu wanaotembea ila ni ngumu kumuona mtu anaetembea kwenye kundi la watu wanaokimbia. -**Chuchu Hans**

# Kuumbe!



# VANESSA WEWE!

## AJIRUSHA KWEUPE NA MNIGERIA

KAMA filamu basi ndio kwanza imeanza! Imeshazoeleka kwa wasanii hawa Jux na Vanessa Mdee, kuanzisha vituko vinavyofananishwa na filamu kila wanapoachana.

Baada ya kuachana kwa mara ya pili, Vanessa ameibuka na jambo jipya ambalo linaweza kumuumiza roho Jux, nalo ni kuanzisha penzi jipya na msanii mwenye asili ya Nigeria anayefanya shughuli zake Marekani aitwaye Rotimi.

Toka habari hiyo isambae kwa kasi mapema wiki iliyopita, Jux hajajitokeza hadharani kuzungumzia na kusababisha mashabiki wao kuwa katika malumbano makali kila upande ukimtetea msanii wao.

Wiki iliyopita Vanessa alichafua hali ya hewa baada ya kuweka picha mtandaoni akionekana akiwa na Rotimi katika mikao ya kimahaba kwenye bwawa la kuogelea huko nchini Marekani wakila bata.

Aidha kama haitoshi wawili hao walirekodi video fupi ikionyesha wakiwa pamoja kupitia Insta Story ya mtandao wa kijamii wa Instagram na hata picha za mwisho walizoposti kupitia mtandao huo mahali ilionesha wakiwa sehemu moja.

Pia kupitia post hizo hizo za Insta Story za mtandao huo wa Instagram Vanessa Mdee alitangaza kuwa sasa hivi atakuwa ana "block"sana watu kupitia mitandao ya kijamii.

**ROTIMI NANI?**

Msanii huyu wa filamu jina lake halisi ni Olurotimi Akinosho, lakini kisanaa anajulikana kama Rotimi.

Kiasili ni mwenyeji wa Nigeria ana miaka 30, makazi yake ameyaweka nchini Marekani.

Rotimi umaarufu wake umekuja baada kucheza vizuri na kubeba uhusika katika filamu mbalimbali ikiwemo ile maarufu duniani iitwayo POWER ambayo imetoka mwendelezo wa msimu wa sita ulianza Agosti mwaka huu.

Filamu zingine alizowahi kushiriki ni kama Deuces, Imperial Dreams na Burning Sands



# Wanamuziki wenye majina ya ndege, wanyama

**Na Adam Fungamwango**

WANAMUZIKI ni watu ambao wanazifanya jamii kupata burudani na kuwafanya wakati mwingine kusahau shida ma mishunguliko ya kutwa nzima.

Muziki ni moja kati ya vitu ambavyo binadamu humfanya kupata tulizo la moyo. Kutokana na wanamuziki kufanya kazi ya kuwatuliza watu na kuwaburudisha, wamekuwa wakipachikwa majina mbalimbali na mashabiki wao kutokana na kuzikubali kazi zao.

Wapiga ala za muziki hasa wa dansi, pamoja na waimbaji wamejikuta wakipewa majina ya utani na mashabiki wao ambayo yamekuwa kama majina yao asilia.

Inafikia wakati hata majina hao halisi husahaulika na badala yake majina yao ya utani waliopewa na mashabiki ndiyo yanayovuma.

Leo tunaangalia wanamuziki waimbaji ambao kutokana na kazi yao nzuri, wakapachikwa majina ya ndege, pamoja na wanyama.

**Hemed Manerti 'Chiriku'**

Huyu ni kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz Band, iliyokuwa maarufu mno katikati ya miaka ya '70, hadi mwanzoni mwa '90.

Alikuwa mwimbaji tegemeo na mtunzi wa bendi hiyo kiasi cha kuifanya kuwa maarufu na wenye mashabiki wengi. Kutokana na umahiri wake, mashabiki wake na wa muziki wa dansi kwa ujumla wakampachika jina la 'Chiriku' wakimfananisha na ndege huyo kutokana na sauti yake na uimbaji wake. Alifariki dunia Mei 31 mwaka 1990 jijini Dar es Salaam kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

**Jerry Nashon 'Dudumizi'**

Ni mtunzi, mwimbaji mahiri wa bendi za Vijana jazz na Bima Lee, bendi ambazo alizitumikia kwa muda mrefu hadi kifo chake mwaka 1995.

Alikuwa mahiri mno kwa nyimbo za mapenzi, akizipamba kwa maneno ya mahaba na ya kubembeleza. 'Nyimbo kama 'Tereza', 'VIP', 'Zaituni', akiwa ba Vijana Jazz na 'Makulatta' akiwa na Bima Lee zilimfanya kuwa maarufu nchini kiasi cha mashabiki kumpachika jina la 'Dudumizi." Hii ni kutokana na sauti yake nzito ya kitetemeshi, iliyofanana sana na ndege huyo ambaye akilia ni kama maji yanamiminwa kwenye glasi. Jina lake halisi lilisahaulika na Dudumizi ndiyo likashika nafasi na hadi leo ili mashabiki wa muziki wamtambue ni lazima umtaje kwa jina la ndege huyo.

**Mohamed Salum 'Gotagota'**

Alikuwa ni mwimbaji wa sauti ya kwanza kali kwenye bendi za Tabora Jazz, Mwenge Jazz na Vijana Jazz. Si wengi wanamfahamu kwa jina lake halisi, ila ukisema Gotagota kila mmoja atajua unamzungumzia nani pamoja na kwamba naye ni marehemu. Alipewa jina hilo alifananishwa na ndege gotagota mwenye mdogo mrefu anayegongagonga miti na kutoa sauti fulani ambayo ndiyo inayofananishwa na uimbaji wa mwanamuziki huyo.

**Nana Njige 'Nana Mzuri'**


Mwimbaji wa kike wa bendi za Super Rainbow, Washirika Tanzania Stars na Magereza. Jina lake ni Nana Njige. Lakini mashabiki wake kwenye muziki wakampajika jina la 'Nana Mzuri'. Nana ni ndege mmoja mwenye wajihi mzuri kwa rangi ya manyoya yake na muonekano. Na alipewa jina hilo kutokana na urembo wake. Mwanamuziki huyo ambaye ameshafariki dunia alitamba sana kwa kibao cha 'Ashura' akiwa na Magereza Jazz.

**Wilson Peter 'Kinyonga'**

Kiuhalisia ni kwamba Kinyonga si jina lalisi la wanamuziki wa Kitanzania, Wilson Peter na mdogo wake Gorge Peter, aliokuwa na bendi ya Jamhuri Jazz ya Tanga, kabla ya kuunda bendi yao ya Arusha Jazz na kuvuka mpaka kuingia nchini Kenya na kuibadilisha na kuiita Simba Wanyika.

Wilson ndiye aliyepewa jina la Kinyonga na mashabiki wake, lakini kutokana na jina hilo kuwa maarufu zaidi, baadhi walidhani ni jina la ukoo kiasi hata mdogo wake George naye kuitwa hivyo.

Kwa hiyo wote wakawa jina la mwisho wanaishia na Kinyonga. Kinyonga ni mnyama mdogo anayefanana na mjusi na anayetembea taratibu na kujibadilisha rangi. Wilson alipewa jina hilo kutokana na kujinasibu kufanya mambo yake taratibu na kwa ufasaha, lakini pia kuwa na uwezo wa kubadilisha muziki wake kama kinyonga anavyojibadilisha rangi ya ngozi yake.



# Vijimambo


1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Kisichoriziki hakiliki

**Na Adam Fungamwango**

TAMAA siku zote ni mbaya. Na kitu chochote ambacho si riziki huwa hakiliki.Kuna baadhi ya binadamu yupo tayari kufanya jambo lolote lile liwe halali au si halali, ili mradi tu aondoke kwenye sehemu moja kwenda nyingine.

Hata hivyo, chochote binadamu hawezi kufanya bila mipango ya Mwenyezi Mungu. Kama hakupanga, hata ufanye nini ni kazi bure tu.

Hii imempata dada mmoja kwenye filamu ya 'Mke Bei Kali.' Huyu amewawakilisha baadhi ya wanawake wenye tabia ya kuwakimbia waume zao na ndoa zao kwa sababu ya shida na umasikini na kwenda ambako anaona maisha yake yanaweza kuwa safi. Hii inatokana na kudanganyika na wapita njia, lakini mara nyingi baadaye yanawakuta makubwa na kushindwa wa kumlilia.

Imechezwa na Irene Uwoya, Simon Mwapagata, Hemed Suleiman, Patcho Mwamba na wengine wengi. Inaanza kumuonyesha Simon anavyoishi kwa amani na mkewe Irene. Kipato chao kikubwa kinapatikana kwa kilimo na kidogo ufugaji. Katika maisha yao, mara kwa mara, mume anamkumbusha mkewe kuwa makini na kujichunga na watu wabaya, wafitini ambao wanaweza kuvunja ndoa yao.

Kwa mastaajabu, siku moja mkewe anatoweka kijijini. Wanakijiji wanakusanyika na kwenda kumtafuta porini kwa kudhani kuwa huenda atakuwa labda ameliwa na wanyama wakali. Mara ya mwisho ilisemekana alionekana anakwenda kuchota maji kisimani.

Wanachofanikiwa kukikuta wanakijiji ni nguo zake badala ya Irene awe hai au amekufa. Baada ya miezi kadhaa kupita, zikaja tetesi kuwa Irene ameonekana mjini.

Taarifa zinakuwa kubwa kiasi cha kuanza kuaminika. Simon anaamua kwenda mjini kumsaka Irene. Wanapofika huko wanaishi maisha ya kubangaiza.

Siku moja akiwa anaangalia televisheni, Simon alimuona Irene akiwa na mwanamuziki maarufu nchini Hemed. Na hapo ikatangazwa kuwa mwanamke huyo ni mke wa Hemed.

Simon hakuamini macho yake. Mkewe leo kageuka kuwa mke wa mwanamuziki mkubwa nchini. Anaulizia anakoishi Hemed. Anafika nyumbani kwake na nia kujua nini kilitokea hadi ikawa hivyo.

Anapofika huko anatimuliwa kama mbwa. Irene licha ya kudai kuwa si mumewe, lakini anasema katika maisha yake hajawahi kuonana na mtu kama huyo.

Simon anaondoka na kuendelea na maisha yake. Irene naye anaanza kuota mapembe. Akaingia mjini kwa pupa na mji ukampokea akaanza kuwa na mahusiano na bosi wa Hemed ambaye ni Patcho Mwamba.

Hakutosheka, akawa kiruka njia haswa. Wakati huo Hemed alikuwa kwenye ziara za muziki. Aliporejea alipata taarifa ya kuwa promota wake ana uhusiano na mkewe. Akamtimua mke na kujiondoa kuwa chini ya Patcho na kuanza kujitegemea mwenyewe.

Irene kwa kuchanganyikiwa alianza kujiingiza kwenye matumizi ya madawa ya kulevya. Mume wa kweli Simon alipopata taarifa akamtafuta mkewe na kumpeleka kwenye kituo cha afya ili kupata tiba. Irene alipopona, alichukuliwa na mumewe Simon na wote wakarejea kijijini kuanza tena maisha mapya



# WAACHENI

## PRINCE HARRY, MEGHAN WAANDAMWA

KWENYE raha kuna karaha! Ndivyo hali inayowakumba wana wa Mfalme Harry na mkewe Meghan Markle kiasi kwamba hivi sasa wanajutia na kupata hofu juu ya maisha yao.

Wanandoa hao ambao wamejizolea umaarufu duniani licha ya kufurahia maisha ya kifalme yenye kila aina ya raha, lakini wameanza kutumbukia nyongo wakilalama wamechoka kufuatwafuatwa.

Prince Harry na Meghan ambaye ana asili ya Kiafrika, katika mahojiano ya pamoja waliofanya na kituo cha televisheni cha ITV wakati wa ziara yao nchini Afrika mapema mwezi Oktoba na kurushwa hewani Jumapili, wamesema hawatakubali magazeti ya udaku ya Uingereza kuwaharibia maisha yao.

Wamelalamika kwamba mambo mengi ambayo yanachapishwa katika magazeti ya udaku siyo ya kweli na yanawachosha.

Prince Harry amediriki kulinganishga hali hiyo na yale yaliyomkuta mama yake Princess Diana kabla ya kufariki dunia kwa ajali ya gari.

"Sitakubali kuingizwa katika hujuma iliyomuua mama yangu." Amesema Harry

Harry amesema bado kumbukumbu ya kifo cha Princess Diana inamsumbua kila siku na kwamba yeye mwenye amejawa na hofu.

Meghan ambaye ni nyota wa zamani wa Televisheni na filamu kutoka Marekani amesema wakati rafiki zake walikuwa na furaha ya yeye kuwa na uhusiano na Harry, marafiki zake wa Uingereza walimuonya kwa sababu magazeti ya udaku ya Uingereza yatamuharibia maisha yake.

Hata hivyo ameelezea namna anavyoweza kukabiliana na ufuatiliaji mzito wa magazeti hayo, "Ukweli ni kuwa nimekuwa kwa muda mrefu nikimwambia Harry haitoshi kuwa utanusurika katika jambo hili, siyo maana ya maisha bali inatakiwa upate mafanikio."

Mapema mwezi huu wanandoa hao walifungua mashtaka dhidi ya gazeti la udaku la Uingereza, The Mail on Sunday kwa kuingilia maisha yao ya faragha kwa kuchapisha barua Meghan aliyomuandikia baba yake.

Kila wakati, Harry analalamika namna wanavyomfanyia Meghan hakuna tofauti na vile magazeti hayo yalivyomfanyia mama yake.

# Burna Boy wasalimie Bondeni



BAADA ya kumalizika kwa vurugu Afrika Kusini, rapa mkali AKA, amethibitisha msanii mwenzake kutoka Nigeria Burna Boy atashiriki onyesho kubwa la muziki likalofanyika nchini humo.

AKA aliandika ujumbe kupitia ukurasa wake wa Tweeter akisema amepata ujumbe kutoka kwa Burna Boy kuwa atawasili kwa ajili ya kushiriki tamasha hilo.

"Burna Boy anakuja Mzansi baada ya kumalizika xenophobia," alitwiti.



## Kanye West unajua kupenda

RAPA mkali wa Marekani, Kanye West, amefanya kufuru baada ya kumzawadia mke wake Kim Kardashian, dola milioni moja kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Mwigizaji huyo wa kipindi kinachoonesha maisha halisi ya wanafamilia wa Kardashian, amepewa zawadi hiyo Octoba 22, mwaka huu ikiwa ni siku yake ya kuzaliwa na pesa hizo zitatumika katika mradi wake wa kusaidia watu waliofungwa gerezani.


"Nashukuru sana kwa mapenzi mazito katika siku yangu ya kuzaliwa, nina raha wakati nikifurahia," aliandika Kardashian.

## Nicki, Petty wafunga ndoa kisiri

NICKI Minaj rapa mwenye matata mengi, imeelezwa tayari amefunga ndoa ya siri na mpenzi wake Kenneth Petty.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ, Minaj na Petty walifunga ndoa jumatatu ya Octoba 21, katika sherehe iliyowahusisha watu wachache na yenye usiri mkubwa.

Kulingana na hati ya ndoa, mwanamuziki huyo amekubali kubadilisha jina kutoka lile la Onika Tanya Maraj na sasa anaitwa Onika Tanya Maraj-Petty.





## Regina ndiyo umefanya nini?

MASHABIKI wa mwigizaji nyota wa Nollywood, Regina Daniel, wamepata kiwewe baada ya akaunti ya Instagram ya msanii huyo kufutwa.

Regina ambaye ana mamilioni ya wafuasi wanaomfuatilia kupitia ukurasa wake, ameufuta jambo ambalo limesababisha wasiwasi kwa mashabiki wake.


Ukurasa huo ulikoma uhai wake Jumatatu ya Octoba 21, na kuibua taharuki katika mitandao ya kijamii huku wengi wakijiuliza kwanini msanii huyo amechukua hatua hiyo ikiwa ana wafuasi wa kutosha wa kumuingizia pesa.

## Tonto kumbe ulijitunza hee!

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, HYPERLINK "https://www.pulse.ng/entertainment/celebrities/tonto-dikeh-shares-shocking-details-of-her-crashed-marriage/5j13n7q" \t "_blank" Tonto Dikeh, amewashangaza mashabiki wake baada ya kuweka wazi kwamba jambo linalomvutia katika mwili wake ni kuwa bikra wakati wa usichana wake.

Tonto Dikeh amesema hayo katika mahojiano na kueleza imekuwa kama miujiza isiyokwisha katika akili yake.

Tonto alijikuta akiweka wazi jambo hilo wakati akijibu maswali 50 aliyoulizwa na mashabiki wake katika mitandao ya kijamii.



SAFU



Na John Juma
0716217615

MIONZI YA SHERIA

# Tujikumbushe kiini cha serikali za mitaa

TUNAPOELEKEA kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji ambao umebakia mwezi mmoja ili kukamilisha jukumu hilo la kikatiba, tunayo mambo ya kufahamu tunapoingia kwenye kazi hiyo ya kuwachagua viongozi hawa.

Ni vyema kufahamu kuwa serikali za mitaa na za vijiji ni chombo cha utawala wa umma, kilichopewa madaraka ya kuamua na kuendesha shughuli zake katika sehemu ndogo ya nchi au taifa ndicho kijiji, mtaa au kitongoji.

Baada ya uhuru, serikali za baadhi ya nchi za Afrika kama vile Zaire au Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Uganda na Senegal zilifuta mfumo wa serikali za mitaa au kubadilisha mfumo wake ulioanzishwa na serikali za kikoloni.

Kwa mfano, serikali ya Tanzania wakati huo haikufuta mfumo huo mara moja. Badala yake ilirithi serikali za mitaa na kuzitumia kama nyenzo za kuleta maendeleo kwa misingi ya kidemokrasia.

Katika kipindi cha miaka ya mwanzo ya Uhuru, yalikuwapo makundi matatu ya serikali za mitaa, la kwanza ni zile zilizoundwa chini ya Sheria Namba 72 ya mwaka 1926 zilizokuwa 47, pili ni zile za chini ya Sheria Namba 333 ya mwaka 1953, zilikuwa tisa kwa mijini na 10 kwa vijijini.

Na kundi la tatu lilihusisha Manispaa ya Dar es Salaam, iliyoundwa kutokana na Sheria Na. 105 ya mwaka 1946, isitoshe, mnamo mwaka 1962 Sheria na 333 ilirekebishwa kwa kuondoa Mamlaka za Wenyeji na mwaka 1963 Sheria Namba 13/62 ilipitishwa kusitisha utawala wa machifu nchini kote nchini.

Halikadhalika, uamuzi wa kufuta utawala wa machifu nchini ulitokana na sababu kuu tatu ambazo ni serikali ya wananchi ilitaka kujenga 'mfumo wa kidemokrasia' wa serikali za mitaa, tena, ilionekana utawala wa machifu uliendeleza fikra za ukabila badala ya utaifa. Sambamba na ukweli kuwa wengi wa machifu hao, siyo wote, walikuwa madarakani kufuatia baraka za serikali ya kikoloni, vibaraka.

Kimsingi, serikali ya wananchi (kwa wakati huo) na sera yake madhubuti juu ya serikali za mitaa, vitongoji na vijiji ilijikita katika kuanzishwa kwa uchaguzi wa madiwani katika halmashauri zote nchini zilizokuwa zimeandikishwa na serikali ya kikoloni; Kuundwa kwa halmashauri katika wilaya au miji ambayo zilikuwa bado hazijaundwa na kuna umuhimu kufanyika hivyo.

**MAFANIKIO**

Mafanikio ya Serikali za Mitaa au Vijiji 1961- 1972 katika kipindi hicho serikali za mitaa na vijiji zilipata mafanikio machache, ukilinganisha na matatizo au changamoto. Kwa mfano majukumu ya halmashauri yaliongezeka kwa kasi sana kama vile usimamizi wa elimu ya msingi, matibabu, barabara na maji.

Na zaidi, halmashauri za wilaya zilikuwa na majukumu mazito zaidi kuliko yale ya halmashauri za miji, ilishangaza kuona bado sehemu kubwa ya ruzuku kutoka serikali kuu ilielekezwa kwenda katika halimashauri za miji badala ya halmashauri za wilaya.

Licha ya hali hiyo ya upendeleo kwa halmashauri za miji, kwa jumla halmashauri za wilaya zilitekeleza majukumu yake vizuri kwa kujikusanyia mapato kutokana na 'kodi' na 'ushuru wa mazao' na wakati huo huo kuhudumia 'miradi mbalimbali ya kuhudumia jamii'.

Katika kipindi husika mapato ya halmashauri yalishuka sana, kushuka kwa uwezo wa halmashauri za wilaya kukusanya mapato ni ishara ya kukumbwa na matatizo katika utekelezaji wa majukumu yake.


Hivyo, halmashauri zikashindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hali hiyo ndiyo iliyojitokeza kwenye serikali nyingi za mitaa, vijiji katika kipindi hicho cha mwaka 1962-1972 ndiyo matatizo yaliyozikabili serikali hizo.

Kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba, serikali za mitaa zilipewa majukumu mara baada ya uhuru na kwamba serikali kuu ilikuwa na nia ya kuleta maendeleo ya haraka kwa watu wake, lakini vyanzo vya mapato kwa serikali za mitaa vilikuwa vichache.

Halmashauri za wilaya, kwa mfano, ziliruhusiwa kukusanya mapato kutokana na kodi na ushuru wa mazao. Ukusanyaji wa kodi kutoka kwa wananchi ulikuwa mgumu, wengi walikuwa wakikwepa kulipa kodi ya kichwa. Jambo hilo lilikuwa kama kero kwao na kusababisha matukio ya aibu na hata maafa. Kutokana na matukio hayo, serikali kuu iliamua kufuta kodi ya kichwa.

Aidha, ilipofika Mei, 1969 ushuru wa mazao nao ulifutwa, uamuzi huo katika masuala mawili uliathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali za mitaa na vijiji nchini. Licha ya kwamba serikali hizo zilitegemea zaidi misaada na ruzuku kutoka serikali kuu baada ya vyanzo kadhaa vya mapato yake kufutwa, pia katika kipindi hicho hicho serikali kuu nayo ilipunguza ruzuku.

**Itaendelea wiki ijayo.**



Na Reubeni Lumbagala

KALAMU YA MWALIMU

# Wadau tumuige Ndugai kufanikisha kambi hizi

KAMBI za kitaaluma ni mpango mkakati unaotumiwa katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi kwenye ngazi mbalimbali za elimu kuanzia wanafunzi wa darasa la saba hadi wa kidato cha sita.

Kupitia kambi za kitaaluma, wanafunzi huishi maisha ya bweni ili kuwapa muda wa kutosha wa kujifunza na kujisomea ili hatimaye waweze kufanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa.

Hapa nchini, wanafunzi wengi wa shule za msingi na sekondari wanasoma katika mfumo wa kutwa ambapo baada ya masomo hurejea nyumbani kwao na kwa walio wengi hakuna kinachoendelea.

Ni wachache tu ambao baada ya kurudi nyumbani hupata muda wa kujisomea yale waliojifunza shuleni. Wengi kutokana na uhuru mwingi walionao nyumbani na kazi za nyumbani hushindwa kujisomea na badala yake hakuna kujikumbusha yale waliojifunza shuleni.

Kutokana na hali hii, wanafunzi wanaoshindwa kujisomea pindi warudipo majumbani mwao huishia kufanya vibaya katika masomo na hatimaye wengi hufeli katika masomo.

Mara nyingi mazingira ya nyumbani kwa wanafunzi wa kutwa huwa si rafiki sana kwa ajili ya kujifunza, kwahiyo, jitihada na utashi wa wazazi na walezi ni lazima uwepo katika kuwahamasisha watoto wa kutwa kujisomea kikamilifu awapo nyumbani.

Kwa kutambua umuhimu wa wanafunzi kuwa na muda wa kutosha wa kujifunza na kujisomea, ndipo suala la kuwaweka kambi wanafunzi hasa wale wa mitihani ya taifa kama darasa la saba, kidato cha pili, nne na sita lilipopewa umuhimu wa kipekee na viongozi na wadau wengine wa elimu katika wilaya mbalimbali hapa nchini.

Wilaya ya Kongwa ni miongoni mwa wilaya ambazo suala la kambi za kitaaluma limepewa kipaumbele na msukumo wa kipekee kwa shule za sekondari. Kambi hizi hufanyika katika shule husika na nyakati za likizo, kambi hufanyika kwa kanda ambapo huwakutanisha wanafunzi wa shule mbalimbali.

Suala la kambi za kitaaluma limesaidia sana kuifanya Wilaya ya Kongwa kung'ara katika Mkoa wa Dodoma na kitaifa katika matokeo ya kidato cha Nne.

Mwaka 2017, Wilaya ya Kongwa ilishika nafasi ya kwanza kwa Mkoa wa Dodoma katika matokeo ya kidato cha Nne na mwaka 2018, Kongwa ilishika nafasi ya pili kimkoa. Haya ni mafanikio makubwa kwani inaonyesha namna viongozi wa serikali, maofisa elimu, walimu, wazazi, walezi na wanafunzi wenyewe walivyo na utayari katika kuisimamia mikakati ya elimu ili kukuza taaluma na ufaulu wa wanafunzi.

Kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa makambi haya, wazazi na walezi kushirikishwa namna ambavyo wataweza kuchangia ili kuwasaidia watoto wao kukaa kambi na hatimaye kupata muda mzuri wa kujisomea.

Niwapongeze wazazi na walezi wa Wilaya ya Kongwa kwa muwa na mwamko wa elimu kwa kushiriki katika kuchangia uendeshaji wa kambi za kitaaluma kwa manufaa ya watoto wao.

Kutokana na manufaa ya kuwaweka wanafunzi kambi, wazazi wanatoa ushirikiano mzuri wa kufadhili kambi hizo.

Mbunge wa Kongwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai ametimiza ahadi yake aliyoitoa mwaka jana ya kuchangia Sh. milioni 10 kutoka Mfuko wa Jimbo, kusaidia kuendeshaji wa kambi za kitaaluma ili kuifanya Kongwa izidi kung'ara kitaaluma. Fedha hizo zinaungana na michango waliyoitoa wazazi na walezi kwa ajili ya uendeshaji wa kambi. Fedha hizo ziligawiwa katika kanda tano ambapo katika kanda ya Mlali ilijumuisha shule za sekondari za Mlali, Manghweta, Chiwe, Iduo na Nghumbi.

Kanda ya Kongwa ilijumuisha shule za sekondari za Sejeli, Kongwa, Mnyakongo, Mumi, Ibwaga, na Sagara. Kanda ya Zoissa ilijumuisha shule za Makawa, Zoissa, Norini, Songambele, Hogoro, Banyibanyi, na Manghaila. Kanda ya Pandambili shule za Ndurugumi, Pandambili, Hembahemba na Laikala. Kanda ya Kibaigwa, shule za Ndalibo, Mtanana, Kibaigwa na Ngomai.

Kila kanda ilipatiwa Shilingi 2,000,000 kwa ajili ya kusaidia chakula na kuwapa posho walimu waliochaguliwa kufundisha kwa muda wa majuma matatu kuanzia Septemba 30 hadi Oktoba 20, 2019. Utekelezaji wa ahadi hii ni matokeo ya Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, kuona namna kambi hizi zilivyosaidia kuipaisha wilaya ya Kongwa kitaaluma na kuwezesha wanafunzi wengi wanaohitimu kidato cha nne kuendelea na kidato cha tano na wengine kuendelea na vyuo mbalimbali vya kilimo, uhasibu, mifugo na ualimu.

Ni ahadi ya Spika Ndugai kuwa ataendelea kufadhili kambi hizi mwaka hadi mwaka, huku walimu, wazazi na wanafunzi wakiwa na deni la kusaidia kukuza ufaulu.

Wito wangu kwa wadau wengine wa Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma na Tanzania kwa ujumla kusaidia mahitaji ya uendeshaji wa kambi kama vile, mahindi, maharagwe, mchele, mafuta, unga, sukari, nyama, kuku chumvi na fedha taslimu ili kambi hizo zifanyike kwa mafanikio makubwa mwakani. Tafakari.

**Maoni: (+255) 764 666349.**

# PETS yaweza kuwa tiba kudhibiti ufisadi

**Na Sabato Kasika**



Baadhi ya wadau wa elimu Wilaya ya Ruangwa wakifuatilia mafunzo ya mradi wa PETS. **PICHA: SABATO KASIKO**.

MIONGONI mwa mambo ambayo baadhi ya wananchi hawayaelewi ni ukweli kuhusu fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Inavyoelekea wengi hawafahamu kuwa fedha hizo ni zao na wanawajibika kuzifuatilia, kuangalia thamani ya kazi na pia kuhoji pale wanapoona kuna mushikeli.

Wengi hawajui kuwa kufuatilia matumizi ya rasilimali zikiwamo fedha ni haki yao kikatiba na kwamba, kuacha kufanya hivyo ni sawa na kuwaachia watu wachache waamue juu ya hatma ya maendeleo na maisha yao.

Moja kati ya njia nyepesi na shirikishi inayoweza kutumiwa na wananchi hata wa kawaida kujua matumizi ya rasilimali za umma zikiwamo fedha ni kwa kutumia mfumo wa ufuatilia rasilimali za umma maarufu kama PETS.

Maneno haya manne 'PETS' ni kifupi cha Public Expenditure Tracking Systems or Survey, mfumo huu umeanzishwa kwa lengo la kuwapa wananchi uwezo wa kufuatilia matumizi ya fedha na rasilimali nyingine za umma ili kuhakikisha kila fedha au mali inayoelekezwa katika miradi ya maendeleo inatumika kikamili.

Changamoto hiyo ya kujua matumizi ya fedha za umma inatokana na ukweli kuwa baadhi ya watu hawaelewi umuhimu wa kufuatilia rasilimali za umma, hilo linabainika baada ya asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (Akuvikiru) kufanya utafiti.

Uchunguzi huo ulifanywa na asasi hiyo katika baadhi ya maeneo ya Ruangwa kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS), ukihusisha sekondari za kata ya Nkowe, Luchelegwa na Malolo.

**KWANINI UFUATILIAJI?**

Mtendaji Mkuu wa Akuvikiru, Abduli Mitumba, anasema serikali imeanzisha utaratibu wa ushirikishwaji wa umma katika kupanga, kutekeleza na kusimamia mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ile ya bajeti, pia imeridhia mfumo wa utawala bora unaotoa fursa ya uwazi wa uwajibikaji kwa viongozi na watendaji wa umma.

Anasema, mfumo huo pia unaainisha mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ile ya bajeti ikianzia ngazi ya chini kwenda juu ikiwamo ya kijiji, kata, halmashauri, mkoa hadi taifa.

"Hapa ina maana wananchi ndiyo wenye jukumu la kuamua vipaumbele vya maendeleo vya maeneo yao kabla wataalam wa uchumi wa ngazi ya halmashauri, mkoa na wizara kisekta hawajapanga bajeti katika vigezo vya kitaalam kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi," anasema.

Vile vile Mitumba, anasema, mfumo wa utawala bora unatoa fursa ya wananchi kuchagua na kuchaguliwa nafsi mbalimbali za uongozi, mfumo unatoa fursa ya wananchi kuwawajibisha viongozi na watendaji wa umma wanaokwenda kinyume na misingi ya utawala bora na maadili ya utumishi wa umma.

"Akuvikiru imefanya uchunguzi na kubaini wananchi wengi hawana elimu ya ufuatiliaji wa fedha za umma zinazotengwa na serikali kwa ajili ya maendeleo yao, hivyo asasi imeamua kujikita huko, hasa upande wa elimu," anasema.

Anaongeza kuwa Mradi wa Kuhamasisha Maboresho ya Elimu Wilaya ya Ruangwa Wilaya ya Ruangwa Awamu ya II, ulianza Septemba 2019 na unatarajiwa kukamilika Machi 2020.

Mitumba anasema, katika kipindi chote hicho, asasi yake inatarajia kuhamasisha uwajibikaji wa wananchi katika kuhoji viongozi na uwepo wa matumizi sahihi ya fedha za umma.

Vilevile uwajibikaji wa watendaji katika kushirikisha utekelezaji wa mipango ikiwamo ya bajeti kwenye ngazi ya vijiji na kata ili wananchi wawe na ujasiri wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma (PETS) zinazotengwa na serikali kwa ajili ya maboresho ya sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu.

**MAONI YA WADAU**

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa, Rashidi Namkulala, anasema ujio wa mradi huo ni jambo la kipekee kwa wilaya yake, hasa ikizingatiwa sekondari zilizolengwa zina miradi mingi inayohitaji kufuatiliwa kwa karibu.

"Kama kweli tunataka kufanikisha malengo mazuri ya mradi huu, ni vizuri kila anayehusika atimize wajibu wake, wakiwamo waratibu wenyewe," anasema Namkulala, ambaye pia ndiye Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa.

Kwa upande wake Ofisa Elimu Kata ya Nkowe, Shannel Nchimbi akichangia mjadala, anasema kuwapo kwa taasisi kama Akuvikiru kuna maana kubwa ndani ya Wilaya ya Ruangwa kwa vile miradi ya elimu ina umuhimu zaidi.

Nchimbi aliyekuwa mkuu wa kwanza wa shule ya Sekondari Nkowe, anasema anafarijika kuona sasa imepandishwa hadhi na kuwa ya kidato cha kwanza hadi sita, tena ikiwa ya mchepuo wa sayansi.

Naye Mkurugenzi wa Muungano wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Wilayani Ruangwa (Mmakiru), Wema Chilungo anasema, muungano wake upo tayari kushiriki katika kila tukio kila utakapohitajika.

"Kinachofurahisha ni kwamba taasisi inayoratibu mradi huu ni mwanachama wa Mmakiru, na pia kutofuatilia rasilimali za umma ni sawa na kulitekeleza taifa," anasema Chilungo na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia miongozo ya elimu na sheria ya nchi ili kufikia malengo.

Mwenyekiti huo anasema, kupitia mradi wa 'Kuhamasisha Maboresho ya Elimu ya Sekondari Wilaya ya Ruangwa Awamu ya Pili', sasa unaendelea kwenye baadhi ya maeneo wilayani Ruangwa.

Mradi huo unaendelea ikiwa ni awamu ya pili baada ya ile ya kwanza ya mwaka 2017 iliokamilika mwaka jana, ambayo ilihusisha sekondari za kata tisa za Nambiranje, Chibula, Matambarale, Narungombe, Chunyu, Nachingwea, Makanjiro, Mandarawe na Likunja.

Anasema, mradi wa sasa ulianza kwa kutambulishwa kwa wadau wa elimu wakiwamo wakuu wa idara za maendeleo ya jamii, elimu ya sekondari, maofisa elimu kutoka kata za mradi na watu wenye ulemavu.

"Wadau wengine ni wakuu wa shule za sekondari za Nkowe, Hawa Mchopa, wenyeviti wa bodi za sekondari hizo, viongozi wa dini, maofisa watendaji wa kata na viongozi wa asasi za kiraia za wilayani Ruangwa," anasema.

Mwenyekiti huo anasema, wakati wa utambulisho, waliwasomea wadau hao mpangokazi wa mradi, wajibu na majukumu yao wakati wote na sababu za kuwapo kwa mradi huo katika maeneo yao.

"Tuliwaambia, ziara ya wajumbe wa kamati ya mradi kwenye vijiji 11 vinavyounda kata za mradi, ambako wangeendesha mikutano ya hadhara, kuwakumbusha wananchi wajibu wao katika kuendeleza sekondari na kuchagua wajumbe wa kamati za PETS, ambao ndio watakaopita kila sehemu kufuatilia matumizi ya rasilimali hizo," anasema.

**TANZIA**

# BURIANI JAMES MAPALALA

## ●Mbegu ya mwanzo vyama vingi nchini

Na Michael Eneza

JUZI taifa lilitangaziwa msiba wa mwanasiasa mbobezi nchini, Mzee James Mapalala. Katika namna na sura yoyote ile, ni pigo katika tasnia ya kisiasa nchini.

Kwa muda mrefu, mwanasiasa huyo aliyetangulia mbele ya haki, amekuwa kimya na kulikuwapo taarifa za muda mrefu ambazo si rasmi kuhusiana na kuumwa kwake.

Mapalala, ni kati ya wanasiasa wasiosahaulika katika mtiririko wa historia kwa walioshuhudia na kusikia kuanza harakati za mfumo wa vyama vingi nchini, akiwa katika safu ya mwanzo ya mageuzi yaliyoidhinishwa kisheria mwaka 1992.

Hata hivyo, haiingii katika kundi la awali zama hizo za historia miaka ya 1960, katika waliodai mfumo wa vyama vingi nchini, ambao wamo kina Christopher Kasanga Tumbo, aliyepoteza nafasi ya ubalozi nchini Uingereza. Alirudi nyumbani na kwa kipindi kirefu akazuiliwa kisheria, ikiwamo nyumbani kwake.

Ukimlinganisha na wanaharakati wa kipindi cha Uhuru waliopigania au kutetea mfumo wa vyama vingi, Mapalala alikuwa wa 'kizazi kipya.' Hata hivyo, katika sura nyingine alianza mapema zaidi, kulinganisha walioibuka wakati zama zake. Mfumo wa kiasisa wa chama kimoja umedumu miaka 28 kuanzia 1964.

Itakumbukwa, mjadala wa kisiasa uliokaribisha mageuzi yaliyofungua mageuzi ya kisiasa nchini, yalikuwa katika zama baada ya kutoka kuzuizini kwa mwanamageuzi wa siasa za Afrika Kusini, Nelson Mandela, mnamo Februari 10, mwaka 1990.

Kusini ni eneo ambalo kisiasa nchini, masikio na vitendo vyetu, vilielekezwa huko kwa muda mrefu, pamoja na sehemu zinginenzo za Afrika. Tanzania ilikuwa kitovu cha kuratibu ukombozi wake.

Hayati Mwalimu Julius Nyerere, akiwa bado ni mwenyekiti wa CCM, pia akishika usukani wa mageuzi kimataifa, alitangaza kuwa "si dhambi kujadili uwepo wa mfumo wa vyama vingi vya siasa." Muda mfupi baadaye, serikali ikaunda tume kuratibu hilo, kwa kuzunguka nchi zima kukusanya maoni. Licha ya zaidi ya robo tatu ya maoni kutaka mfumo wa chama kimoja, mapendekezo ya tume chini ya marehemu Jaji Francis Nyalali, yalitaka kufunguliwe mlango wa siasa huru na ndicho kilichotekelezwa.

Hadi muda wa mageuzi unafikiwa, Mapalala alishakuwa tayari mhanga wa harakati hiyo kwa muda mrefu, kwani aliangalia hali inavyokwenda mwanzoni mwa miaka ya 1980 na kufikia uamuzi kuwa kuna hoja ya mabadiliko.

Mapalala alikuwa mjasiriamali, mjenzi wa majumba katika maeneo tofauti, huku akitawaliwana na shauku kubwa ya masuala ya sheria na katiba.

Alianza kudodosa dhana hiyo, akishirikiana na wanasheria kadhaa na kuvunja sheria kwake, kulimuacha aangukie mikononi mikoni mwa dola, mwaka 1984 na alirejea uraiani mdaka 1992.

Inadaiwa, baadhi ya wanasheria alioshirikiana nao wakati huo katika nyendo zilzomponza, alikutana nao tena wakati mfumo wa vyama vingi unaanza rasmi.

Zlikuwa jitihada binafsi zenye washabiki wengi miongoni mwa wasomi, lakini ikawa vigumu hata mmoja wao kutoka hadharani kukiri anashiriki harakati hizo, kwani wengi walitegemea ajira za umma, na kama si hivyo basi kandarasi za serikali; kwa hilo Mapalala alipata shida pia.

Siasa huru zilipoanza rasmi, Mapalala alikuwa katika kundi kubwa la chombo kilichoitwa Kamahuru, kilichoshinikiza mabadiliko hasa kwa siasa za Zanzibar, ikiundwa na wananarakati wa Bara na Visiwani.

Mfumo wa vyama vingi ulipokubaliwa, ilibidi waunde chama na ikaonekana wazi kundi hilo haliwezi kudumu kwa pamoja, likagawanyika. Wanasheria waliosheheni hapo, hawakumchagua Mapalala kuwa mwenyekiti wao, wakampa mwanasheria mwenzao, Mabere Marando.

Hivyo, Mapalala akajirejesha kwa mwenzake aliyekaa kizuizini baada ya kufukuzwa CCM, Maalim Seif Sharif Hamad. Inadaiwa kisiasa 'waliendana' na madhila yao kisiasa yalifanana, ingawa wana historia tofauti; mjasiriamali na mwanasiasa wa damu.

Hivyo Mapalala, alikuwa mwanasiasa wa upinzani asiye na asili, wala mzizi wa kutumikia serikalini, tofauti na wengi ambao wali serikali ay katika chama tawala ma vyombo vyake .

Kisiasa, Maalim Seif aliyewahi kuwa Waziri Kiongozi Zanzibar, amekuwa maarufu zaidi kuliko Mapalala. Ilifika wakati kama zilivyo 'ligi'za kisiasa ndani na nje ya chama, walisuguana na Mapalala akajikuta anawekwa nje ya chama - CUF.

Ndani ya hatua zake zote, Mapalala hakuujua ubunge au uwaziri, bali alikuwa mwananchi aliyepigania kuleta mageuzi kisiasa, yakaja halafu akawekwa pembeni na mikiki ya siasa hizo.

Msingi wa umaarufu wa Maalim Seif kama mtu aliyekuwa kizuizini na jina lake likapaa sana Zanzibar, ulitosha kumfunika Mapalala, hasa Zanzibar.

Umaarufu kama huo wa kuwezesha kukakmata siasa, Bara ulidakwa na wanasiasa walioubuka kama kina Christopher Mtikila za 'sisi Watanganyika,wao Wazanzibari.,' Waliopangana kufuatana na vigezo vya aina hiyo na Mapalala akjukta tena'wa kuja' katika hadhara zao.

Itakumbukwa zama zile siasa za mageuzi zimenoga akiwa CUF, Mapalala hakuwahi kuwa na matukio ya kuitisha, mfano maandamano au hadhara makubwa katika vwanja vya Jangwani, Dar es Salaam, kulikokuwa maarufu kwa mikutani ya kisiasa. Kitabia alikuwa mtu mtulivu wakati wote.

Alipofikuzwa, baadhi ya wafuasi wake wa CUF, waliendana naye hadi kuunda Chama cha Haki na Ustawi (Chausta), lakini wakati huo nguvu zikawa zimemwishia na rasilimali za kuenedesha siasa zikiwa zimeyeyuka.


Baada ya ukimya mrefu, ndipo aliitwa katika Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014, mjini Dodoma na baadaye akawa katika ukimya mrefu, hadi taarifa ya umauti.

**MUNGU AIWEKE ROHO YAKE MAHALI PEPONI. AMINA.**



Hayati Mzee James Mapalala. **PICHA: MTANDAO.**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 17 00)



Dondoo: Kulia

1. Mji mkuu ni Maputo
6. Mbinu
8. Mtu anayetafsiri Lugha
10.Tunda lenye mibamiba
11.Maksi
13. Sehemu ya kushikia jembe 14.Kiungo katika mboga 17. Tinga
21. Iliyopita kiwango cha kawaida 22. Nyumba ya Wamasai 23. Jongea mahali
25. Tunda a mbamia
26. Fadhila
27. Vunjia mtu heshima

Dondoo: Chini

1. Enzi
2. Udugu
3. Kati ya
4. Neno la kutilia mkazo
5. Mfugaji wa Arusha
7. Ndoto ya kutisha
9. Teketeza
12.Hufunga na kufungua mango
15.Taarifa
16. hali ya kuchukizwa na
18. Mwanamitindo Tanzania
19. Neno la kuuliza
20. Aibisha
24. Ndugu wa kike

Jibu Na: 16






Ofisa wa Maji Bonde la Wami/Ruvu, Simon Ngonyani, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni kuhusu ulipaji wa tozo ya mwaka kwa watumiaji wa maji chini ya ardhi na juu ya ardhi kulia ni hilo Arorld Kayoza. **PICHA: FRANK MONYO.**

# Mnaodaiwa mabonde sikilizeni kilio hiki

**Na Frank Monyo**

HIVI karibuni Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, imetishia kupeleka mahakamani wamiliki wa hoteli 73, kampuni 13 na vituo vya mafuta 14 , wanaotuhumiwa kukaidi kulipa ada ya mwaka ya watumia maji ya visima ambayo ni Sh. milioni 33.

Ofisa wa Bonde la Wami/Ruvu, Simon Ngonyani, ndiye aliyetoa taarifa hiyo mbele ya wanahabari na kueleza kuwa ofisi yake imeshatoa notisi ya madai kwa wamiliki hao 100 ambapo baadhi yao mpaka sasa walemilipa Sh. milioni 49.

Ngonyani anasema kuwa ulipaji wa ada hizo ni muhimu kwani husaidia bodi kutekeleza shughuli za utunzaji wa rasilimali za maji zitakazohakikisha upatikanaji wa maji kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kutimiza azma ya nchi kufikia uchumi wa viwanda.

Vilevile anasema kuwa ulipaji wa ada za matumizi mbalimbali ya maji ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 kifungu cha 43 (1) ambacho kinamtaka mtu yeyote anayetaka kuchepusha, kukinga, kuhifadhi, kuchukua na kutumia maji kutoka kwenye chanzo cha maji juu ya ardhi au chini ya ardhi au kujenga miundombinu yoyote lazima aombe kibali cha kutumia maji hayo.

Anazitaja baadhi ya hoteli ambazo zinadaiwa mpaka sasa kuwa ni Africa Sana, Iceland, J&P, KB, Lunchtime li, Mambosasa, BnB , Confidence, Don Lodge na Grand Villa.

Kwa upande wa vituo vya mafuta ni TSN Oil, Gapco (T) Ltd, Mantrac (T) na Lake Group au Lake Oil, wakati nyingine ni Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Dar es Salaam, Shule ya St. Marry's na Alpha Paints zote za Dar es Salaam.

Ngonyani anazungumzia gharama akisema ada ya mwaka kwa kisima cha matumizi madogo nyumbani ni Sh100,000 na matumizi makubwa ya biashara ni Sh150,000 na kwa wafugaji wa samaki.

Anaeleza kuwa ombi la kuchimba kisima ni Sh. 60,000 huku ada yake kwa mwaka ikiwa ni Sh100,000 kwa matumizi madogo na Sh 250,000 kwa matumizi makubwa.

"Tulikuwa na jitihada za kuwatafuta watu ambao walikuwa hawalipi ada za matumizi ya maji ya visima, na wapo wachache ambao tumewapeleka mahakamani kwa kukaidi takwa la kisheria la kulipa ada za watumia maji ya visima na wakalipa, huku wengine wakiahidi kulipa pasipo utekelezaji. Wateja hawa lazima tuwashughulikie," anasema Ngonyani.

Kutokana na hilo, Nipashe ilishuhudia wamiliki wa visima vya biashara na vya nyumbani wakiwa wamejitokeza ofisi za bonde hilo zilizopo Ubungo kupata maelekezo ya namna ya kulipia ada hizo.

Pamoja na muitikio huo, inaonyesha dhahiri kuwa baadhi yao hawana elimu juu ya umuhimu wa kufuata taratibu za uchimbaji kisima pamoja na kulipia ada zake kwa mwaka.

Mmoja wa wadau aliyemwakilisha mmiliki wa hoteli moja jijini Dar es Salaaam ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini anasema kuwa kabla ya kufika hapo alikuwa haelewi, wametumia gharama zao wenyewe kuchimba kisima kwanini walipe tozo za mwaka serikalini?

"Bosi wangu amenituma nije hapa ofisini kuulizia taratibu na kulipa ada ya mwaka ambayo tunadaiwa, unajua mimi nilikuwa sielewi inakuwaje kisima tuchimbe sisi halafu hela tulipe serikalini? Lakini baada ya kupewa elimu hapa nimeelewa kwanini yatupasa kulipa," anasema

Ngonyani anaeleza kuwa yapo madhara makubwa yanayoweza kujitokeza endapo watu hawatafuata utaratibu wa kuchimba visima kutoka kwa wataalamu wa bonde linalohusika.

Anasema kuwa athari ya majengo makubwa kuanguka kutokana na uchimbaji holela wa visima hasa kwa wamiliki wa hoteli, vituo vya mafuta na kampuni ni kubwa kama hawatafuata utaratibu uliopo.

"Sisi ni wataalamu ndiyo maana tunawashauri kwamba ni lazima wafuate utaratibu kwani kuchimba visima kiholela si jambo zuri kwa afya zao na mali zao pia waje waombe vibali ili tuweze kufahamu nani anachimba wapi kwa sababu tutachimba hadi kwenye mashimo ya choo na matokeo yake ni hatari kwa afya zao pia," anasema Ngonyani

Anaongeza kuwa watu ambao wanachimba visima kiholela hasa kipindi hiki cha mvua wanakuwa katika hatari za kupata magojwa ya mlipuko kwani uchafu unaosombwa na maji ya mvua unaweza kupelekwa hadi kwenye visima kutokana na kutochimbwa kitaalamu.

**Vilevile anasema kuwa ulipaji wa ada za matumizi mbalimbali ya maji ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 kifungu cha 43 (1) ambacho kinamtaka mtu yeyote anayetaka kuchepusha, kukinga, kuhifadhi, kuchukua na kutumia maji kutoka kwenye chanzo cha maji juu ya ardhi au chini ya ardhi au kujenga miundombinu yoyote lazima aombe kibali cha kutumia maji hayo.**

"Kumekuwa na sintofahamu baada ya tamko la serikali mwaka huu juu ya kufuta tozo za matumizi ya maji ya visima vya nyumbani, hivyo kusababisha watumia maji hasa wamiliki wa hoteli, nyumba za kulala wageni, vituo vya mafuta na makampuni kukaidi ulipaji wa tozo za maji za visima," alisema Ngonyani na kuongeza:

"Nataka kusisitiza kuwa tozo iliyofutwa ni ada za mwaka za matumizi ya maji ya visima vya nyumbani iliyokuwa Sh. 100,000 kwa mwaka kwa kila kisima kwa shughuli za nyumbani tu na siyo kuuza maji au visima vilivyopo eneo la biashara."

Anasema kwa wale wamiliki wa hotel, vituo vya mafuta, nyumba za kulala wageni na makampuni ambao hawajalipa tozo za maji wanapaswa kulipa ili kuepuka kupelekwa mahakamani.

"Nia yetu ni njema tu hatutaki kukimbizana na kupelekena mahakamani kwani tukipata hizo fedha tunakuwa na uwezo wa kusimamia rasilimali za maji kwa siku zijazo kwa faida ya nchi na vizazi vijazo.," anasema Ngonyani

# Kilichokubalika Urusi na Afrika

**SOCHI, Urusi**

RAIS wa Urusi Vladimir Putin, ameongoza mkutano wa kwanza kati ya Urusi na Afrika uliohitimishwa juzi Alhamisi, katika mji wa pwani wa Sochi.

Mkutano huo, ulilenga kuisaidia Urusi kuimarisha ushawishi wake barani Afrika katika masuala ya usalama na biashara.

Rais Putin aliahidi kuongeza mara mbili kiwango cha uwekezaji barani Afrika baada ya kuafikiana kuhusu masuala mbalimbali:

Kwa upande wa masuala ya kijeshi na siasa, Urusi ilitia saini mkataba na serikali ya Nigeria, ili kuiuzia helikopta 12 aina ya Mi-35 Hind E.

Aidha, Urusi inapanga kuuza silaha zenye thamani ya dola bilioni nne katika nchi mbalimbali barani Afrika mwaka huu wa 2019.

Putin pia alisema tayari Urusi, imesamehe deni la dola bilioni 20 kwa mataifa mbalimbali barani Afrika.

Halikadhalika, Urusi pia iliahidi kusaidia kumaliza mizozo nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan.

Kwa upande wa nishati kampuni ya serikali ya Urusi iliahidi kujenga vinu vya nyuklia kwa lengo la kuzalisha umeme nchini Ethiopia.

Benki ya kitaifa nchini humo na kituo cha uwekezaji nchini humo vimetia saini mkataba na Serikali ya Congo Brazaville kujenga bomba la mafuta.

Katika hatua nyingine , imetia saini makubaliano na serikali ya Morocco kuisaidia katika kusafisha mafuta ghafi.

Kwenye uchumi na biashara, benki kubwa inayotoa mkopo Sberbank, VEB na kituo cha usafirishaji kimeshirikiana na kituo cha uwezekaji jijini London Gemcorp, itatoa dola bilioni tano kusaidia uwekezaji katika mataifa ya Afrika.

Mkataba huo utasaidia kutoa msaada wa fedha katika nchi ya Angola, Ethiopia, Msumbiji na Zimbabwe.

Kuhusu mipango ijayo kati ya Urusi na Afrika, ilibainika kuwa uwekezaji kati ya Urusi na Afrika imeongezeka mara mbili kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na kufikia zaidi ya dola bilioni 20.

Aidha, kiwango cha biashara kuongezeka mara mbili kwa kipindi cha miaka minne na mitano ijayo ni jambo lililokuwa na kipaumbele pia.

Hata hivyo baadhi ya wachambuzi, wanaona kuwa Urusi bado ipo nyuma katika utoaji wa misaada na uwekezaji barani Afrika, nyuma ya Umoja wa Ulaya-EU inayotoa dola bilioni 334 kila mwaka kwa ajili ya masuala ya biashara, huku China ikitoa dola bilioni 204.

Mtalaam wa masuala ya Urusi, Samuel Ramani kutoka Chuo Kikuu cha Oxford, alisema Urusi inataka kushawishi zaidi barani Afrika na kuuza bidhaa zake katika mataifa mbalimbali barani humo.

Katika mkutano huo uliomalizika Sochi, Alhamisi wiki hii masuala mbalimbali ya kiuchumi yalijadiliwa.

Rais Vladimir Putin na viongozi wa Afrika pia walijadili changamoto za vita dhidi ya ugaidi barani Afrika na msaada wa Moscow hasa katika eneo la Saheli au mzozo wa Libya.

Tangu mwaka 2017, Urusi imetia saini mikataba ya ushirikiano wa kijeshi na nchi 20 za Afrika, na inatarajia kuendelea katika mwelekeo huo.

Vladimir Putin, anataka kuonekana kama msaada unaowezekana katika vita dhidi ya ugaidi katika bara hilo na kuzuia majaribio yoyote ya mapinduzi ya serikali za Kiafrika. Hayo aliyoiweka wazi katika kikao cha mjini Sochi.

***RADIO UFARANSA***



Rais wa Urusi, Vladimir Putin (anayepunga mkono), akiwa na viongozi wa Afrika katika mkutano wa Afrika na Urusi, uliomalizika hivi karibuni mjini Sochi. **PICHA: REUTERS.**

# Chama tawala

**Botswana chashinda**

CHAMA tawala nchini Botswana cha Democratic - BDP kimeshinda uchaguzi mkuu baada ya kupata viti 29 katika bunge la taifa, ikiwa ni sawa na asilimia 51 ya kura.

Wananchi wa Botswana walipiga kura siku ya Jumatano wiki hii kulichagua bunge la taifa lenye viti 57 na wawakilishi 490 wa serikali za mitaa, wakati mgombea wa chama kitakachoshinda ndiye atakuwa rais. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Terrence Rannowane, alisema kuwa licha ya kwamba bado zoezi la kuhesabu kura linaendelea, idadi ya wabunge ilichopata chama cha BDP inamlazimu kumtangaza Mokgweetsi Masisi, kuwa rais mteule wa Botswana. Chama kikuu cha upinzani, Umbrella for Democratic Change, UDC, kimepata viti 13 wakati chama cha Botswana Patriotic Front kimeshinda viti vitatu na chama cha Alliance for Progressive kimepata kiti kimoja, huku asilimia 73 ya majimbo ya uchaguzi tayari yakiwa yamekwisha hesabiwa.

***DW***



Rais wa sasa, Mokgweetsi Masisi, ambaye chama chake kimepata ushindi wa kishindo. **PICHA: MTANDAO.**

# Daktari matatani kisa mtoto kazaliwa bila uso

**SETUBAL, Ureno**

DAKTARI mmoja nchini Ureno amesimamishwa kazi baada ya mtoto kuzaliwa bila pua, macho na sehemu za kichwa.

Wazazi wa mtoto Rodrigo hawakuwa na ufahamu kuhusu maumbile hayo ya mtoto wao hadi alipozaliwa mapema mwezi huu.

Maofisa wa baraza la madaktari waliamua kumsimamisha kazi daktari Artur Carvalho kufuatia madai ya uzembe.

Ilibainika kwamba malalamiko mengine zaidi yanayohusu watoto wengine yaliyofanyika zaidi ya muongo mmoja iliyopita pia yamewasilishwa mbele ya baraza hilo.

Ripoti ya visa hivyo, zilizoelezewa na vyombo vya habari vya Ureno imezua hisia kali. Daktari Carvalho hajajibu tuhuma dhidi yake.

Rodrigo aliyezaliwa Oktoba katika hospitali ya Sao Bernardo mjini Setubal, takriban kilomita 40 kusini mwa Lisbon, mama yake alikuwa chini ya uangalizi wa daktari Carvalho akipigwa picha mara tatu katika kipindi cha ujauzito.

Huduma hiyo ilitolewa katika kliniki moja ya kibinafsi na wazazi hao wanasema kwamba daktari huyo hakuonyesha wasiwasi wowote kuhusu afya ya mtoto huyo akiwa tumboni.

Mama huyo baadaye alifanyiwa uchunguzi wa skana yenye maelezo zaidi kwa kutumia mfumo wa 5D katika kliniki tofauti akiwa na ujauzito wa miezi sita.

Wakati wa skana hiyo uwezekano wa mtoto huyo kuwa na umbo lisilo la kawaida uliwasilishwa , lakini daktari Carvalho alidaiwa kupuuza hofu iliyojitokeza kufuatia uchunguzi huo mpya wa kina

Alinukuliwa akielezea kwamba mara nyingine wakati wa utafiti baadhi ya sehemu za uso wa mtoto wao akiwa tumboni zilikuwa hazionekani , hasa wakati uso wa mtoto umeshikana na tumbo la mama, shangazi lake Rodrogo , aliielezea AFP.

Baada ya kuzaliwa kwa Rodrigo na umbo lake lisilo la kawaida kubainika, wazazi wake waliambiwa ataishi kwa saa chache.

Hatahivyo baada ya wiki mbili , mtoto huyo bado yuko hai chini ya usimamizi wa hospitali.

Wazazi wake wamewasilisha malalamishi kuhusu Daktari Carvalho Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Ureno.

BBC

# HADITHI

# Jumba Jekundu-24

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

Siku ya tatu ilikuwa imepita. Maisha yalikuwa yakiendelea kama kawaida. Hakukuwa na dalili yoyote ile kama kungekuwa na kitu chochote kibaya mabacho kilitegemewa kutokea kwenye familia ya kina Kadili.

Walishangazwa na hilo. Timbwili la mama Pauline wanalitambua vema. Mama anatambua jinsi alivyo mwepesi wa kutuma mabaunsa.

Kadili anajua ubabe, ufedhuli, jeuri na ukatili na Mama Pauline. "Inawezekana labda wamempata." Hilo ni wazo ambalo lilimjia Kadili baada ya kuona inapita siku ya tatu na tayari ilishakuwa jioni bila dalili ya askari wala mabaunsa.

"Hodi." Sauti ya ghafla ilisikika na kumshtua Kadili.

Hata hivyo, ilikuwa ni sauti ya mtu ambaye anamfahamu. Ni Meze, hivyo wasiwasi ulipungua.

Akili nyingine ikamjia kuwa huenda akawa ameongozana na watu wengine.

Taratibu alinyanyuka kwenye kochi na kwenda kufungua mlango.

Mikono ilikuwa inatetemeka. Pamoja na yote alitegemea yanayokwenda kutokea. Akafungua.

"Vipi mbona umetoa macho namna hiyo." Meze alimuuliza rafiki yake.

"Mimi nilijua ndiyo tayari hivyo nakuja kuchukuliwa."

"We acha woga bwana, kwani sauti yangu huijui?"

"Kwani kuijua tatizo? Unaweza ukaja nao, wakakukuta huko wakakuuliza ukaja nao."

"Eee ndugu yangu kazi unayo, maana unaishi kiuwogauwoga kama jambazi."

"We acha tu, sijui yataisha mwaka gani."

"Eee bwana mimi sikuja kukaa, ila kukupa taarifa tu."

"Taarifa gani wewe Meze mbona unaendelea kunitisha? Nahitajika kwenye kituo cha polisi nini?"

Kikazuka kicheko cha ghafla kwa wote wawili.

"Eee maana tuambizane mapema." Kadili alidakia baada ya kumaliza kicheko chake.

"Hapana nimekuja kukupa taarifa ya msiba."

Taarifa hiyo ilimshtua Kadili kwani hakutegemea kuambiwa kitu kama hicho, dakika moja tu baada ya kuwa kwenye kicheko.

Mshangao mwingine ni kuwa hakumuona rafiki yake Meze akiwa kwenye majonzi yoyote wakati alipofika.

"Huu ni msiba wa nani?" Alijiuliza na baadaye akauliza kwa sauti "Nani amefariki?"

"Mama Edina amefariki?" Ilikuwa ni sauti ya Meze iliyopenya vema kwenye masikio ya Kadili.

"Mama Edina gani?" Lilikuwa ni swali tata ambalo hata mweyewe Kadili hakujua aliliuliza kwa sababu gani.

"Kwani wewe unamjua mama Edina gani?"

"Mama Pauline."

"Ndiyo huyo huyo amefariki?"

Mama Pauline, mama mzazi wa Edina anayemtambua yeye ni mwanamke wa makamo, shupavu, tajiri, anayejiamini, mjivuni, mwenye dharau, katili, mkali na mwenye vitisho.

"Wewe nani kakwambia?" Lilikuwa ni swali lingine aliloulizwa Meze.

"Nimesikia kwenye redio wametangaza, lakini jinsi walivyokuwa akiongea wanavyomuongelea na wewe ulivyonieleza, nikajua ni huyo huyo."

"Unajua siamini Meze, Madame Pauline amefariki. Kwa nini?"

"Nimesikia ugonjwa wa moyo. Ila tusiandikie mate na wino upo, saa hizi karibu saa 10:00 alasiri wanaweza kurudia tena kwa habari kwa ufupi tunaweza kusikia, fungulia redio." Meze alishauri.

****************************

Kama ilivyo ada. Habari kwa ufupi ilianza ilipotimu saa 10:00 alasiri. Moja ha habari ilikuwa ni ya kusikitisha ilitangazwa redioni.

'Habari kutoka Dar es Salaam, inasema kuwa mama mmoja mfanyabiashara maarufu nchini Pauline Barton, maarufu kama mama Pauline, amefariki dunia jana usiku nyumbani kwake Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda ya Kinondoni, amesema kuwa mama huyo amefariki kwa ugonjwa wa moyo.

Hii imekuja wiki moja tu baada ya binti yake Edina Barton kutoweka nyumbani kwa mumewe Dk. Deus Kapilima maeneo ya Mbezi Beach jijini Dar es Saalaam.

Kamanda akaongeza kuwa huenda mama huyo alipatwa na mshtuko kutokana na habari za binti yake kutoroka kwa mumewe na hadi sasa hajaonekana alipo. Mwisho wa habari kwa ufupi.'

Ilikuwa ni taarifa fupi, lakini iliyojitosheleza kwa Kadili. Hakuhitaji nyongeza ya maneno ili kujua kuwa Mama Pauline, mwanamke aliyemuogopa kama ukoma amefariki dunia.

Hakujua ahuzunike au afurahi. Hakujua baada ya hili nini kitaendelea. Huenda kifo cha Madame Pauline kinaweza kusababisha urahisi wa yeye kumpata Edina? Wazo hilo aliliondoa kwa sababu hakukuwa na makubaliano au kitu chochote ambacho awali kilionyesha kuwa yeye na Edina wana dalili za kuwa wapenzi, zaidi ya kucheza muziki pamoja, pia urafiki ya kuongea na kufahamiana, ingawa ndani ya moyo wake alikuwa amempenda msichana huyo.

Utofauti na hali, yeye akiwa fukara hohe hahe na Edina kutoka kwenye familia ya kitajiri pia ulikuwa kikwazo kwake.

Kwa upande mwingine kifo cha Pauline kinaweza kuwa ni chanzo cha misukosuko kwake na kuonekana kwa familia ya mama huyo kuwa huenda yeye ndiye aliyesababisha hayo. Hili halikumuondoka kichwani.

Kama alikamatwa na kupelekwa kwenye jumba jekundu la hayati mama Pauline na kuteswa, akateseka kwa kitu ambacho hakukifanya na hakipo, familia haiwezi kushindwa kudhani kuwa anahusika.

Kitu kingine kilichomuuliza ni kujua alipo Edina. "Yuko wapi?" Alichokuwa na uhakika ni kwamba Edina atakuwa amemtoroka mume kwa sababu aliozwa bila ridhaa yake. Aliozwa kwa nguvu tu na mama yake na hakuwa anampenda mume huyo. Mama alitaka tu binti yake aolewe na mtu tajiri, mwenye uwezo, msomi au vyote kwa pamoja, lakini si mtu fukara ili mradi tu mwenyewe binti amependa.

"Amekimbilia wapi? Anaishi kwa nani?" Hili ni swali lililomtesa moyoni mwake.

"Inawezekana Edina ana mwanaume ambaye anampenda na ametorokea huko anaishi kwake?" Aliwaza na kujiuliza mwenyewe. Kwa mbali wivu ulianza kumuingia.

Yoyote atakayekuwa mpenzi wa Edina atakuwa mtu mwenye maarifa sana, akisaidiwa na binti huyo kwani yeye hajulikani kwao na hata marehemu Madame Pauline hakujua chochote kuhusu mtu huyo na badala yake yeye Kadili ndiye mtu wa kusukumiwa mzigo kuwa ndiye anayemharibu Edina wakati si kweli.

Pamoja na yote hayo, wazo la kwenda Oysterbay kwenye msiba halikuja kabisa. Alijua akitia pua yake tu, anawezwa kubebwa msobemsobe ama na madausa au na polisi kwa kusababisha kifo cha mama hiyo, kwani huenda wakajua kuwa Edina anaweza kuwa alitorokea kwake.

Pia hakuwa na uhakika kuwa binti huyo atakuwepo msibani kwani taarifa inasema kuwa tangu atoroke kwa mumewe hajaonekana. Ina maana hata nyumbani kwao hakwenda ndiyo maana mama yake akapatwa na mshtuko, hivyo hana uhakika kama atakuwepo kwenye msiba, au atasubiri kwanza sakata liishe ndipo arudi nyumbani kwani kwa msiba huu, Edina ana hatia ya kusababasha umauti wa mama yake, ingawa hawezi kukamatwa na polisi, lakini machoni mwa waombolezaji, ndugu na jamaa ataonekana ni 'muuaji' aliyesababisha kifo cha mama yake bila kukusudia.


Maswali yamekuwa ni mengi kwake kuliko majibu. Kadili alionekana kutatizwa na mambo mengi yaliyompata tangu alipokamatwa na kupelekwa kwenye jengo hile, mateso aliyoyapata, alipotoka, kuolewa kwa Edina, kutoroka kwa mumewe hadi kifo cha mama Pauline, lakini hakuwa na mtu wa kumuuliza.

Aliyakumbuka maneno ya kifedhuli ya marehemu mama Pauline, lakini pia na baadhi ya yale yaliyomburudisha.

Kuna kitu kimoja tu ambacho kilimpa faraja.

"Nisikilize kwa makini. Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama. Nadhani ulitembezwa kwenye yale makaburi ya wajinga wenzako. Kuanzia leo sitaki umfuatilie tena mwanangu. Umuogope kama ukoma. Sitaki kusikia habari zako tena hapa. Nikisikia chochote kile juu yako na binti yangu, au kutoa siri ya hiki kilichomo kwenye nyumba hii, basi tusilaumiane. Kwa sababu ni lazima uuawe." Yalikuwa ni maneno ya Mama Paulime siku za nyuma alipokamatwa na kupelekwa kwenye jumba lake Oysterbay.

***Itaendelea Jumamosi***



# KEANA AMTAKA KANE UNITED



**MANCHESTER, England**

GWIJI wa Manchester United, Roy Keane ameitaka klabu yake hiyo kumsajili mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane.

Keane mapema wiki iliyopita wakati akichambua pambano kati ya Man United dhidi ya mahasimu wao Liverpool, alidai njia ya mkato ya Kocha Ole Gunnar Solskjaer kutatua tatizo la ushambuliaji ni kumnunua Kane.

"Ni rahisi tu, nenda kamnunue Harry Kane kutoka Spurs. Nenda ukamnunue Kane. Kwani naamini Kane atakuwa msaada mkubwa kwa Man United," alisema Keane.

Hata hivyo, kauli hiyo imepokewa tofauti na Solskjaer pamoja na beki wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Stuart Pearce ambao wamesema si kazi rahisi kumsajili Kane.

"Kwa washambuliaji ambao tunao, nasubiri kwa hamu kuona kitakachotokea wiki chache zijazo. Hakuna washambuliaji wengi sokoni kama (Robert) Lewandowski na Harry Kane.

Wao wapo kama (Alan) Shearer, (Ruud) Van Nistelrooy ni wafungaji mahiri. Wakwetu ni tofauti, lakini naweza kusema napenda mtu ambaye anaweza kumalizia nafasi ngumu. Kane ni mmoja kati ya wafungaji bora, lakini ni mchezaji wa Tottenham," alisema Solskjaer.

Wakati Solskjaer akisema hayo, Pearce alidai kwa sasa si rahisi kwa United kumchukua Kane kwa sababu mvuto wa timu hiyo umeondoka.

"Unapotazama zamani hivyo ndivyo ambavyo Sir Alex alikuwa anapenda kufanya. Alifanya kwa Van Nistelrooy, Cole, Sheringham, Berbatov. Alizoea kwenda kumnunua mshambuliaji bora aliyekuwa anapatikana wakati huo," alisema Kane.

Mpaka sasa United imefunga mabao kumi katika mechi tisa za Ligi Kuu ya England na hivyo kuonyesha wazi kuna matatizo katika safu hiyo ya ushambuliaji.

Hayo yanatokea wakati Kocha Solskjaer akiwa amewaruhusu mastaa wawili wa zamani wa United, Romelu Lukaku na Alexis Sanchez kuondoka kikosini hapo katika dirisha kubwa lililopita la majira ya joto.

Mpaka sasa Rashford ndiye anayeongoza kwa kufunga mabao katika kikosi cha United katika ligi akiwa amefunga mara nne wakati kinda Daniel James aliyenunuliwa kutoka Swansea akiwa na mabao matatu.

Hii inamuacha Solskjaer akiwa anasaka mshambuliaji wa kati kuongeza makali katika kikosi hicho.

## LIVERPOOL YAJITOSA KUMSAJILI SANCHO

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool sasa imeingia kwenye mbio za kuisaka saini ya winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

Liverpool bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, wanataka kuimarisha kikosi chao kwa kumsajili winga huyo wa timu ya Taifa ya England.

Klabu yake ya Dortmund ambayo imeanza kuingiwa na hofu, mara kadhaa imekuwa ikisisitiza kwamba, Sancho hauzwi.

Sancho alifungiwa na kupigwa faini baada ya kuchelewa kurejea klabuni akitokea kuitumika timu yake ya taifa na jambo hilo limeonyesha kumkera kijana huyo.

"Nilichosikia ni kwamba Liverpool imedhamiria," chanzo kimoja kutoka ndani ya Liverpool kilinukuliwa na Lverpool.

"Naamini katika dirisha la mwishoni mwa msimu watakuwa moja ya timu zenye nafasi kubwa ya kumsajili," aliongeza.

## GUARDIOLA AMFUATA RUIZ WA NAPOLI



**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City wameendelea na mbio zao za kumsaka kiungo mahiri wa Napoli na timu ya Taifa ya Hispania, Fabian Ruiz.

Miamba hao wa pale kwenye dimba la Etihad mapema wiki hii walituma maskauti kwa ajili ya kumfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Kocha wa City, Pep Guardiola anamuona Ruiz kama kiungo mwafaka wa kuchukua nafasi ya staa wake mkongwe wa Hispania, David Silva ambaye ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu baada ya kucheza Etihad kwa miaka 10.

Hata hivyo, City watalazimika kukumbana na wakati mgumu kutoka kwa klabu mbili kubwa za Hispania Real Madrid na Barcelona ambazo pia zinamtaka staa huyo ambaye alitajwa kuwa mchezaji bora wa Euro chini ya umri wa miaka 21 katika dirisha kubwa la majira ya joto mwaka jana.

Fabian aliitwa kwa mara ya kwanza kuiwakilisha timu ya taifa ya wakubwa ya Hispania na kocha Luis Enrique Machi 15, 2019.

## HABARI MICHEZO




# DROGBA

## AMPA MANE TUZO BALLON D'OR 2019

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane anastahili kushinda tuzo ya Ballon d'Or 2019 baada ya kuwa kwenye kiwango kizuri kwa kipindi cha miezi 12 katika klabu na nchi yake, kwa mujibu wa Didier Drogba.

Mane aliiongoza katika mechi zote 13 Liverpool kwenye kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na alimaliza kuwa mmoja wa wafungaji bora wa Ligi Kuu ya England wakati timu yake ikikosa kutwaa taji kwa pointi moja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alisaidia Senegal kufika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika, ambapo walifungwa kwa bao 1-0 na Algeria.

Mane ameanza msimu wa 2019-20, kwa kiwango cha kuvutia na wiki hii aliorodheshwa katika orodha ya wachezaji 30 wanaowania tuzo ya Ballon d'Or pamoja na wachezaji wenzake sita kutoka Liverpool.

Na Drogba ambaye ni mchezaji wa zamani wa Chelsea sasa anaona kwamba, Mane anastahili tuzo hiyo.

"Kwa Kombe la Mataifa ya Afrika, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England (Mane anastahili kushinda)," alisema Drogba.

"Kile anachokifanya kwenye Ligi Kuu, ni wachezaji wachache zaidi wenye uwezo wa kufanya hivyo."

George Weah ndiye mchezaji pekee wa Afrika ambaye ameshinda tuzo hiyo, akiitwaa mwaka 1995, na Drogba anaona sasa ni zamu ya Afrika tena.

"Kuna wachezaji wengi ambao wameliwakilisha vizuri bara la Afrika, kama Samuel Eto'o," alisema.

## Rivaldo ampa Mbappe njia kumfikia Messi, CR7

**PARIS, Ufaransa**

RIVALDO anaamini Kylian Mbappe "lazima aondoke" Paris Saint-Germain kwenda Ligi Kuu ya Hispania, La Liga au Ligi Kuu ya England ili kuweza kujithibitishia yeye mwenyewe kwamba yupo kwenye daraja sawa na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Mbappe amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora duniani, akivaa medali akiwa na Monaco na PSG, huku pia aliisaidia Ufaransa kutwaa Kombe la Dunia mwaka 2018.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 - ambaye ametajwa kwenye orodha ya kuwania tuzo ya Ballon d'Or - ameendelea kuhusishwa na miamba wa La Liga, Real Madrid.

Wakati Rivaldo akiwa na shaka juu ya nafasi ya klabu yake ya zamani ya Barcelona kumsajili Mbappe, amemtaka Mfaransa huyo kuondoka PSG ili kutimiza ndoto zake.

"Nafikiri kwamba itakuwa ngumu kwa Barcelona kumsajili kwa siku za usoni, huku akiwa mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi na kijana, pamoja na hadhi ya kubeba Kombe la Dunia, inamfanya kuwa



mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani," alisema Rivaldo akiiambia Betfair.com.

"Kama Barca wamepata matatizo makubwa zaidi kujaribu kumsajili Neymar, fikiria ni kiasi gani PSG watataka ili kumuuza Mfaransa huyo, na ni kama vigumu mno kumsajili mchezaji kwenda pale Catalunya.

"Hakuna shaka kwamba, Mbappe ana ubora wa kuweza kuwa mchezaji bora duniani, hasa akiwa anacheza soka la kuvutia.

"Naweza kujiimarisha zaidi kwa kipaji chake kama akienda La Liga au Ligi Kuu ya England. Ligue 1 kwa uhakika kabisa ushindani wake ni mdogo ikilinganishwa na Hispania na England.

"Kwa heshima ya PSG, naamini anatakiwa kuondoka kwenda Hispania au Uingereza ili kuweza kufika kwenye daraja moja na Messi au Ronaldo. Wachezaji bora wanahitaji kucheza kwenye ligi bora."

Mbappe alitokea benchi na kufunga mabao matatu, 'hat-trick' wakati PSG ikiifumua Club Brugge mabao 5-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne.

Nyota huyo wa PSG sasa amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga mabao 15 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na umri wa miaka 20 na siku 306 akiivunja ile ya Messi - ambayo aliiweka akiwa na umri wa miaka 21 na siku 288.

Mbappe amefunga mabao sita kwenye mashindano yote msimu huu kwa kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel.

## Maswali hukusu Ozil yamvuruga Emery

**LONDON, England**

UNAI Emery aliachwa amevurugwa na maswali ya waandishi wa habari kuhusu majaliwa ya Mesut Ozil hapo Arsenal baada ya uamuzi wake wa kumuacha kiungo huyo kwenye mchezo dhidi ya Vitoria SC, Ligi ya Europa.

Ozil amewachezea mara mbili tu 'Washika Bunduki' hao wa London, akianza dhidi ya Watford na Nottingham Forest kwenye Ligi Kuu ya England na Kombe la EFL.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, bado hajaitwa kwenye mchezo wowote wa Ligi ya Europa, wakati Emery akiendelea kutomjumuisha.

Lakini alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Ozil wakati Arsenal ikibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Vitoria Alhamisi, Emery alikataa kulijibu swali hilo.


"Nafikiri huu si muda wa kuzungumza kuhusu hilo," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari.

"Ningependa kuzungumzia kuhusu mechi na kuhusu wachezaji waliocheza.

"Hakuwapo kwenye kikosi na hayo yalikuwa maamuzi na sasa tunaangalia mchezo unaokuja wa Jumapili dhidi ya Crystal Palace."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PEPE AMKOSHA EMERY AKIIOKOA ARSENAL EUROPA

Ni mchezaji mzuri na tunamwamini kabisa, alijaribu wiki iliyopita kwa kupiga faulo wakati wa mazoezi...

**LONDON, England**

Unai Emery amempongeza Nicolas Pepe baada ya mabao yake mawili ya faulo ndogo yaliyoipa Arsenal ushindi kwenye mechi ya Europa League dhidi ya Vitoria Guimaraes, akiyaita "kamili".

Winga huyo wa kimataifa wa Ivory Coast aliingia akitokea benchi dakika ya 74, kuchukua nafasi ya Alexandre Lacazette, na kuiwezesha Arsenal kushinda kwa kutupia mabao mawili ya faulo ['free-kicks'] dakika ya 80 na 92 katika ushindi wao wa 3-2.

Kilikuwa ni kiwango ambacho kilipongezwa na Emery, ambaye alifunguka kuwa Pepe amekuwa akifanya mazoezi ya kupiga faulo wakati wa mazoezi.

"Kila mchezaji mpya kawaida anahitaji muda wa kuzoea," alisema katika mkutano na wanahabari. "Pepe ni mchezaji mzuri na tunamwamini kabisa.

"Tuwenye furaha sana kwake na sisi kwa sababu ana mabao mawili faulo mbili ambazo ni kamili. Alijaribu wiki iliyopita kwa kupiga faulo wakati wa mazoezi na nilitazama namna alivyopiga.

"Anaimarika na usiku wa leo [juzi] amefunga mabao mawili, ambayo ni muhimu kwetu na kwake. Anaendelea kuzoea na mapema atakapozoea hilo ni bora kwetu.

"Kitu muhimu ni pointi tatu na kwamba wachezaji binafsi wanaweza kuimarika, hilo linaweza kumfanya kujiamini na kwao."

Arsenal walianza kufungwa kabla ya Pepe kuingia uwanjani, na Vitoria walikuwa wazuri zaidi, lakini Emery anaamini kikosi chake hatimaye kilistahili ushindi na kisha kikatokea nyuma kikiwa kimelala 2-1 na kushinda mabao 3-2 katika Uwanja wa Emirates juzi usiku.

"Mengi yametokea ndani ya dakika 90," aliongeza. "Europa League ni muhimu kwetu na lengo letu kumaliza wa kwanza katika kundi. Katika kipindi cha kwanza, tulihangaika sana kuliko tulivyohitaji, tulipoteza mipira mingi katikati na kuwa na nafasi ya kufunga na kuanza kushinda mechi.

"Kipindi cha pili tulimiliki mchezo vizuri na tulikuwa na nafasi nzuri... nadhani tulistahili kushinda, lakini Vitoria walicheza vizuri. Kila timu ya Ureno ni timu zilizoandaliwa sana, wanamuundo mzuri na wachezaji wazuri.

"Kuna vitu vingi chanya kuliko hasi na ninataka kuchukua vitu chanya usiku wa leo kwa ajili ya mechi zijazo."

## KWA UFUPI

**RODWELL, ROMA WAJIFUNGIA**
KIUNGO wa zamani wa Manchester City na England, Jack Rodwell, 28, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru, yupo katika mazungumzo na Roma kuhusu kujiunga na miamba hiyo yaSerie A. ***(Mail)***

**EMERY MBOGO KWA OZIL**
KOCHA wa Arsenal, Unai Emery alikataa kujadili kwa nini amemwacha Mesut Ozil nje ya kikosi chake kilichocheza mechi ya Europa League dhidi ya Vitoria Guimaraes juzi, Alhamisi. (Mirror)

**MULLER AWINDWA UNITED**
Manchester United inavutiwa kwenda kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich, Mjerumani Thomas Muller, 30, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Bild, via Star)***

**BAYERN YAMKANA MOURINHO**
MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc amepuuzia tetesi kuwa kocha wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Jose Mourinho atapewa jukumu la kuinoa klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Germany, via Mirror)***

**CHILWELL, MADDISON BADO UTD**
Manchester United haina uwezekano wa kumsajili beki wa Leicester City, Muingereza Ben Chilwell, 22, ama kiungo James Maddison, 22, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Manchester Evening News)***

**CHELSEA YAMUWINDA WERNER**
Chelsea imeongeza kujiamini kwamba kufungiwa kwa klabu hiyo kusajili kutafutwa na inatazama uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth na England, Callum Wilson, 27, na straika wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, 23. ***(Sun)***

**EVERTON YAHAKIKISHIWA SIDIBE**
Monaco haitamuita beki Mfaransa Djibril Sidibe, 27, kutoka Everton anapoichezea kwa mkopo wa muda mrefu, kufuatia tetesi kwamba klabu hiyo ya Ufaransa inataka kuvunja mkataba huo hapo Goodison kwa sababu AC Milan inahitaji huduma yake***. (Liverpool Echo)***

**SLIMANI RUKSA MONACO**
Monaco ina kipengele kinachoiruhusu kumnunua mcheza kwa mkopo klabuni hapo akitokea Leicester, straika Mualgeria Islam Slimani, 31, na chanzo kimoja cha nje kimesema ada yake ni robo ya pauni milioni 29 ambazo 'Mbweha' hao walilipa wakati wakimnunua mwaka 2016. ***(Sky Sports)***

**SCHOLES AMTAKA OZIL UNITED**
Paul Scholes anaamini klabu yake ya zamani, Manchester United inapaswa kujaribu kumsajili kiungo asiyekubalika Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil, 31, ili saidie kutatua matatizo katika safu yao ya ushambuliaji. ***(BT Sport, via Evening Standard)***

**DE BOER CHUPUCUPU UNITED**
KIUNGO wa zamani wa Uholanzi, Ronald de Boer, 49, angeweza kujiunga na Manchester United mwaka 2000, lakini alishauriwa kuhusu hilo na kocha Mholanzi Louis van Gaal, ambaye alienda kuinoa United mwaka 2014. ***(FourFourTwo)***

**LEICESTER YAHUSISHWA NA BAYKUS**
Leicester imekuwa ikihusishwa na kiungo wa Trabzonspor, Mturuki Kerem Baykus, 19. ***(Fotospor - in Turkish)***

**NAPOLI KWA IBRAHIMOVIC**
RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema anavutiwa kumsajili Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye atakuwa mchezaji huru dirisha dogo la usajili la Januari wakati mkataba wake na LA Galaxy

HABARI MICHEZO

# LIGI YA WANAWAKE KUANZA KURINDIMA LEO

Na Shufaa Lyimo

LIGI Kuu ya Wanawake ya Serengeti Lite inatarajiwa kuanza kutimua vumbi leo katika viwanja sita tofauti.

Viwanja vitakavyotumika kesho kwa ajili ya ligi hiyo ni ule wa Karume ambapo Simba Queens itaialika Ruvuma Queens, wakati ule wa Jamhuri Baobab Queens ikiwa na kibarua kigumu dhidi ya JKT Queens, huku Shikh Amri Abeid jijini Arusha, Tanzanite Queens ikiwa mwenyeji wa Yanga Princess.

Uwanja mwingine ni ule wa Nyamagana ambao utatumika kwa mechi kati ya Alliance Girls na Kigoma Sisters, wakati Gwambina utatumika kwa mchezo kati ya TSC Queens dhidi ya Marsh Queens na katika Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani Mlandizi Queens itaialika Panama Girls.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Soka la Wanawake, Amina Karuma, alisema timu zote zitacheza kesho na kwamba maandalizi yamekamilika.

Naye Ofisa Masoko wa Kampuni ya Serengeti George Mango, alisema wataendelea kuidhamini Ligi ya Wanawake kwa sababu kwa sasa imekuwa na mwamko mkubwa.

# MSUVA AZIDI KUKIMBIZA WAKITINGA NUSU FAINALI

Na Mwandishi Wetu

KIUNGO mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva amezidi kung'ara ughaibuni baada ya kuifungia timu yake ya Difaa Hassan El-Jadida bao la tatu ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Chabab Atlas Khenifra katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Morocco juzi usiku.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Ben Ahmed El Abdi mjini El Jadida, Mazghan, Msuva ambaye ni mchezaji wa zamani wa Klabu ya Yanga alifunga bao hilo dakika za majeruhi wakati wakiongoza 2-0.

Mabao mengine ya Difaa Hassan El-Jadida yenye mchezaji mwingine Mtanzania, Nickson Kibabage aliyesajiliwa kutoka Mtibwa Sugar, yalifungwa na El Mehdi Karnass dakika ya 49 na Bilal El Magri dakika ya 82.

Kwa ushindi huo nusu fainali sasa Jadida inaungana na Hassania Agadir iliyoitoa Ittihad Tanger, Tihad Casablanca iliyoitoa Ittihad Khemisset na Moghreb Tetouan yenye kiungo Mtanzania, Maka Edward aliyetokea Yanga pia iliyoitoa Rapide Oued Zem.

Kiwango cha Msuva kimezidi kuimarika tangu ajiunge na Difaa Hassan El-Jadidi, na kuimarika kwake kuwekuwa msaada mkubwa katika kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars pindi anapoitwa kuitumikia.

Kama ilivyo kwa Msuva, Watanzania pia wanamatarajio makubwa ya kuona Kibabage naye anaimarika na kumvutia Kaimu Kocha wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije kumjumuisha katika kikosi chake.

WALETENI HAO...



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Singida United itakayopigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kesho, Jumapili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam yapania kujipoza kwa Ruvu Shooting

Na Shufaa Lyimo

BAADA ya kupoteza mechi iliyopita ya Ligi Kuu Bara timu ya Azam FC imepania kutofanya makosa tena itakapokutana na Ruvu Shooting kesho kwenye muendelezo wa ligi hiyo ambayo mabingwa watetezi, Simba wapo kileleni.

Mechi iliyopita, licha ya Azam kuonyesha kandanda la kuvutia, ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Simba kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Jumatano wiki hii.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Azam, Idd Cheche alisema kikosi chake kinaendelea vizuri kwa ajili ya mchezo huo na kufafanua upungufu uliyojitokeza mechi iliyopita wanaendelea kuufanyia kazi.

"Kikosi chetu baada ya kumaliza mchezo wetu dhidi ya Simba, tumeanza mikakati ya kwenda kupambana na Ruvu Shooting," alisema Cheche.

Alisema anashukuru mpaka sasa hana majeruhi hata mmoja ambaye anaweza kuukosa mchezo huo kutokana na kutokuwa fiti kucheza.

"Nashukuru mpaka sasa sina majeruhi hata mmoja, wachezaji wote wapo sawa kukutana na Ruvu Shooting," alisema Kocha huyo.

Aliwataka mashabiki wao wasikatishwe tamaa na matokeo waliyoyapata dhidi ya Simba na badala yake wagange yajayo kwa kutazama mechi zinazowakabili.

Azam iliyoshuka dimbani mara nne hadi sasa, imeendelea kubaki na pointi zake tisa baada ya kupoteza mchezo wao dhidi ya Simba ambayo leo itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Singida United kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

## Ubalozi wa Uholanzi kushindanisha wapigapicha

Na Mary Geofrey

UBALOZI wa Uholanzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, umeandaa mashindano ya picha ya dunia mwaka 2019 (World Press Photo) za mnato na video ambazo zitashindanishwa kwa kuzingatia vigezo vya kutoa habari zenye uzito na muonekano bora na zinazozingatia usahihi na ubora.

Balozi wa Uholanzi nchini, Jeroen Verheul, akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu mashindano hayo, alisema yataanza Oktoba 25 na yanatarajiwa kumalizika Novemba 14, mwaka huu katika ukumbi wa Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa jijini Dar es Salaam.

Alisema katika shindano hilo, picha za habari zilizopokelewa kutoka sehemu mbalimbali duniani zaidi ya 78,801 za wapiga picha 4,738 kutoka nchi 129 zitashindanishwa.

Alisema mbali na shindano hilo pia watakuwa na maonyesho ya picha duniani yatakayohusisha picha 140 zilizochaguliwa.

"Warsha hizi zitatoa fursa kwa wapigapicha za habari na waandishi wa habari ambao wamechaguliwa kujadili na kutafakari kuhusu taaluma zao na fursa zilizopo nchini za uandishi wa habari kwa lengo kuu la kuamsha ubunifu na kukuza mijadala kuhusu masuala ya dunia pamoja na nafasi ya vyombo vya habari kama majukwaa yanayowezesha watu kubadilishana taarifa," alisema Balozi Verheul.

Alisema picha zilizoshinda tuzo mwaka jana zitaonyeshwa wakati wa maonyesho kwenye miji zaidi ya 100 na nchi 45.

Naye Mkufunzi wa Picha, Mwanzo Millinga, alisema washiriki watаelezwa kuhusu namna ya kutuma picha zao na kukidhi vigezo na masharti ya kushiriki katika mashindano ya picha ya habari ya dunia (World Press Photo).

Aidha, aliwataka wapigapicha kutumia Mfuko wa Picha za Habari za Ulimwengu wanaotumia picha kujisajili katika kanzidata ya Waandishi wa Habari wa Afrika (APJD).

# Michezo

Jumamosi Oktoba 26, 2019
Nipashe



Pepe amkosha Emery akiiokoa Arsenal Europa

HABARI UK 30

JUU KWA JUU...




Wachezaji wa Arsenal, straika Gabriel Martinelli na kiungo Joe Willock katika harakati za kufunga kwenye mechi ya Europa League wakati wakishinda 3-2 kwa mbinde dhidi ya Vitoria Guimaraes ambayo ilipigwa Uwanja wa Emirates juzi. **HABARI UK. 30**

# YANGA YAJIMWAMBAFAI, PYRAMIDS WACHEKELEA

●●●Waarabu hao watua CCM Kirumba na kusema mbona uwanja tu, Zahera asema kazi imekwisha...

**Na Focus Nicus**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga wamejimwambafai [wamejigamba] kufanya kweli kwenye mechi yao ya mchujo dhidi ya Pyramids FC ya Misri ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayopigwa kesho katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Hata hivyo, wakati Yanga ikijimwambafai kufanyia kazi mapungufu yaliyokuwapo kwenye safu ya ushambuliaji, wapinzani wao Pyramids wametua jijini Mwanza na kuuchekelea Uwanja wa CCM Kirumba kuwa katika hali nzuri tofauti na walivyodhania awali, huku wakichagua kujifua katika dimba la Nyamagana.

Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera aliliambia Nipashe kuwa ana matarajio makubwa ya kikosi chake kufanya vizuri katika mchezo huo kwa kuwa tayari ameshafanyia kazi mapungufu yaliyokuwa yakiiandama timu yake hususan safu ya ushambuliaji.

Alisema safu yake ya ushambuliaji ilikuwa ikishindwa kutumia vema nafasi walizokuwa wakizitengeneza jambo ambalo lilikuwa kikwazo kwao kupata ushindi mnono katika mechi zilizopita.

"Tatizo la washambuliaji wetu walikuwa hawaangalii kwanza nafasi aliyopo kipa pindi wanapopata nafasi wakiwa na mpira, tulikuwa tunapiga tu mipira bila kumwangalia kipa, hilo sasa tumelifanyia kazi na tunaweza kupata matokeo.

"Tunauhakika tunaweza kutengeneza tena nafasi kwani Jumatatu si Jumanne na wala Jumanne haiwezi kuwa Jumatano na Jumatano pia haiwezi kuwa Juamasita [Alhamisi]," alisema Zahera. Kuhusu kukosekana kwa Maybin Kalengo kutokana na kuwa majeruhi, Zahera alisema hana hofu katika nafasi hiyo kwa kuwa atatafuta mshambuliaji mwingine mwenye kasi ambaye anaweza kuziba nafasi hiyo na kuisadia Yanga kupata matokeo.

Naye nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi, alisema wamejiandaa vema kupata matokeo na wanachohitaji kwa sasa ni sapoti kutoka kwa mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kesho.

"Tumejiandaa vema na walimu wameshafanya kazi yao, tunaweza kupata matokeo hivyo, mashabiki wakijitokeze kwa wingi kutupa sapoti kesho," alisema Tshishimbi.

Kwa upande wa viongozi wa Pyramids ambao walitangulia kutua nchini na kwenda moja kwa moja jijini Mwanza kabla ya timu yao kutua usiku wa kuamkia jana, walitembezwa Uwanja wa CCM Kirumba na kuuona kabla ya kupewa fursa ya kuchagua uwanja wa mazoezi na kuchagua ule wa Nyamagana.

Akizungumzia mapokezi yao, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema awali Pyramids walikuwa na hofu kuwa wamepelekwa 'machinjioni' Uwanja wa CCM Kirumba, lakini baada ya kufika na kukagua eneo la kuchezea na kuzungusha Mwanza kujionea mazingira ya jiji hilo, walifurahia na kuchagua kufanyia mazoezi Uwanja wa Nyamagana.

"Viongozi wao walitangulia jijini Mwanza tumewazungusha hapa jijini ikiwa ni pamoja na kuwapa fursa ya kuchagua uwanja wa mazoezi kabla ya siku ya mwisho kwenda kufanya mazoezi CCM Kirumba, na wameuchagua Nyamagana.

"Kwa ujumla wamefurahishwa na mazingira na hali ya hewa ya jiji zima la Mwanza ikiwa ni pamoja Uwanja wa CCM Kirumba itakapochezwa mechi," alisema Bumbuli.

## 'Msiowapenda wanarudi Simba'

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI kamili la kikosi cha Simba sasa linakaribia kukamilika baada ya beki mwenye mapafu 'mithili ya mbwa' kutokana na pumzi kali ya kupanda na kushuka, Mohamed Hussein 'Tshambalala' pamoja straika anayesifika kwa kuwa na jicho la goli, John Bocco kurejea 'mdogomdogo'.

Bocco amekuwa nje tangu Agosti 25, mwaka huu alipoumia wakati wa mechi ya raundi ya awali dhidi ya UD Songo ya Msumbiji iliyopigwa Uwanja wa Taifa na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, akiungana na Tshabalala aliyeumia hivi karibuni akiwa katika majukumu na timu ya Taifa, Taifa Stars.

**Jana wachezaji hao ambao wamekuwa chachu ya ushindi katika kikosi cha Stars, walikuwa wakifanya mazoezi mepesi pamoja na kocha wa viungo wa timu hiyo wakati wachezaji wenzao wakiendelea kujifua kwa nguvu kwenye mazoezi yaliyokuwa yakiendelea viwanja vya Gymkhana.**

"John Bocco na Mohamed Hussein wanaendelea na mazoezi mepesi. Hivi karibuni watakuwa wamepona na kuendelea kuwapa burudani Wanasimba," ilieleza taarifa ya Simba.

Simba iliyopo kileleni mwa Ligi Kuu Bara baada ya kushinda mechi zake zote tano ilizocheza hadi sasa, itashuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kesho kuivaa Singida United kwenye muendelezo wa ligi hiyo.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >